epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Ijumaa Novemba 22, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MIAKA 30 Nipashe
www.ippmedia.com
ISSN 0856 • Na. 0581868
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

## KAMPENI ZAKOLEA...

# CCM wapeana tahadhari, Lissu aibuka kisera zaidi



“Kijiji kina madini lakini katika akaunti ya kijiji hakuna hata mia mbovu, maana yake uongozi uliokuwapo madarakani umeshindwa kusimamia maslahi ya wakazi wa kijiji hiki...

**DOYO HASSAN - NLD**



“WanaCCM wasifurahie migogoro inayofukuta ndani ya vyama vya upinzani au kusambaratika kwa vyama hivyo. Vyama hivyo ni muhimu kwa maendeleo ya taifa.

**JOHN MONGELLA**



“Nchi haikombolewi kwa maombi, haikombolewi kwa kupiga magoti na kumwomba Mungu, inakombolewa kwa mapambano, fanyeni kampeni, mkafanye uchaguzi...

**TUNDU LISSU**



“Miaka mitano iliyopita, uchaguzi kama huu tunaofanya ulivurugwa, watu wakapitishwa bila kupingwa, wakatangazwa kuongoza vijiji na mitaa yetu bila ridhaa yenu. Mwaka huu figisu zipo...

**ZITTO KABWE**

UKURASA 2&3

UKURASA WA 4

**12** kutoa ushahidi kesi anayedaiwa kutishia kuua kwa bastola klabuni

UKURASA WA 7

KUCHOMA MKE KWA MKAA
**Mshitakiwa** aomba mahakama isipokee barua ya kukiri kosa

UKURASA WA 19

**Russia** yajibu mapigo ya Ukraine kwa makombora ya masafa marefu

UKURASA WA 21



**BRUNO AFICHUA KUTAKIWA MAN CITY**

## Ubomoaji jengo lililoporomoka Kariakoo waanza, Kamati Uchunguzi nayo yazinduliwa

UKURASA 4



## MIKOPO MTANDAONI...

# Benki Kuu: Wakopeshaji hawa 69 nchini hatuwatambui

UKURASA 2

**MICHEZO** **MOALLIN AJIPANGA KUIPAISHA YANGA** UK.24

**KATUNI** UK.6

MIKOPO MTANDAONI...

# Benki Kuu: Wakopeshaji hawa 69 hatuwatambui

**Na Mwandishi Wetu**

MWEZI mmoja baada ya Nipashe kutoa ripoti kuhusu utoaji mikopo holela unaofanywa mtandaoni, Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imetangaza orodha ya watoa huduma 69 wasiokuwa na kibali ambao hawaruhusiwi kutoa huduma za mikopo mtandaoni.

Oktoba 21 mwaka huu, Nipashe ilichapisha ripoti ya uchunguzi, ikionesha madhila wanayokutana nayo wakopaji mtandaoni, huku BoT ikieleza kuwa haiwatambui kisha ikatoa mwongozo na kuwataka wajisajili ndani ya siku 14.

Licha ya BoT kutoa mwongozo huo na kuagiza wajisajili, ni watoa huduma wanne tu walijitokeza kusajiliwa ambao Benki Kuu haijawaweka wazi.

Taarifa kwa umma iliyotolewa jana na Gavana wa BoT, Emmanuel Tutuba, ilibainisha kuwa: "Benki Kuu ya Tanzania inapenda kufahamisha umma kuwa imebaini kuwapo kwa majukwaa na programu tumizi (applications) zinazojihusisha na utoaji mikopo kidijitali bila ya kuwa na leseni na idhini kutoka Benki Kuu ya Tanzania."

Kupitia taarifa yake hiyo, Gavana Tutuba alisema majukwaa na programu hizo zimeshindwa kukidhi matakwa ya Mwongozo kwa Watoa Huduma Ndogo za Fedha wa Daraja la Pili wanaotoa huduma za mikopo kwa njia ya kidijitali wa mwaka 2024 uliotolewa na BoT.

"Mwongozo huo unalenga kuimarisha usimamizi wa Watoa Huduma Ndogo za Fedha Daraja la Pili nchini na kuhakikisha uzingatiwaji Kanuni za Kumlinda Mlaji wa Huduma za Fedha, ikijumuisha uwazi, uwekaji tozo na riba, njia za ukusanyaji madeni, na utunzaji taarifa binafsi za wateja na kulinda faragha zao," alisema.

Gavana Tutuba alisema, "Kupitia taarifa hii, Benki Kuu ya Tanzania inapenda kuarifu umma kwamba majukwaa na programu tumizi zifuatazo hazina kibali na haziruhusiwi kuendelea na shughuli za utoaji mikopo kidijitali.

"Applications hizo ni BoBa Cash; Hewa Mkopo; Money Tap; Soko loan; Bolla Kash Financial Credit; Hi Cash; Mpaso Chap Loan-Mkopo Kisasa; Sunloan; BongoPesa-Personal Online Loan; HiPesa; Mun loan; Sunny Loan na Cash Mkopo.

"Wengine ni Jokate Foundation Imarisha Maisha; My credit; Swift Fund; Cash pesa; KOPAHAPA; Nikopeshe App; TALA; Cash poa; Kwanza loan; Nufaika Loans; TikCash; CashMama; L-Pesa Microfinance; Okoa Maisha - Mkopofast na Twiga Loan.

"Wengine ni CashX; Land cash; Pesa M; TZcash; Credit Land; Loanplus; Pesa Rahisi; Umoja; Eaglecash TZ; M-Safi; PesaPlus 64. Usalama Na Uwakika Mkopo Dk15; Fast Mkopo 29.

"Wengine ni Mkopo Express; PesaX ; Ustawi loan; Flower loan; Mkopo Extra; Pocket loan; Viva Mikopo Limited; FUN LOAN; Mkopo haraka; Pop Pesa; VunaPesa; Fundflex; MkopoFasta; Premier loan; Yes Pesa; Get cash.

"Wengine ni MkopoHaraka; Safe pesa; ZimaCash; Getloan; Mkopohuru; SasaMkopo; Getpesa Tanzania; Mkoponafuu; Silk loan; Hakika loan; Mkopowako na Silkda Credit."

Gavana Tutuba alisema BoT inatahadharisha umma kutojihusisha na majukwaa na programu tumizi hizo na inashirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuzifungia programu hizo ili kuepusha umma kutumia huduma za fedha zisizokuwa na vibali vya mamlaka husika.

"Benki Kuu Tanzania imechapisha na itaendelea kuhuisha orodha ya watoa huduma walioidhinishwa kutoa huduma za mikopo katika tovuti yake," alisema Gavana.

Katika tovuti ya BoT, kumewekwa pia orodha ya watoa huduma ndogo za fedha waliosajiliwa 1,957 na 12 ambao wamenyang'anywa leseni kwa kushindwa kukidhi matakwa ya leseni zao.

Walionyang'anywa leseni kwa maeneo wanayotoka na idadi kwenye mabano ni Shinyanga (1), Kinonndoni (4), Ilala (3), Ubungo (2), Arusha (1) na Karatu (1).

Katika uchunguzi wake, Nipashe ilibaini watoa mikopo mtandaoni, wengi wao ni waliosajiliwa na BoT kama watoa huduma ndogo za fedha (microfinace) ambao wanamiliki programu tumizi.

Nipashe ilibaini wanatoa mikopo yenye riba kubwa inayofika hadi asilimia 80, masharti ya mikopo yanafichwa, udhalilishaji wakopaji kwa kuundiwa makundi katika mitandao ya kijamii kisha picha zao kusambazwa na matumizi ya namba za simu zenye utambulisho (code) usiotambulika.

Nipashe pia ilibaini vijana wenye umri mdogo wamekuwa wanatumika kutukana na kudhalilisha wakopaji kwa njia ya simu, kutuma na kusambaza picha chafu zilizotengenezwa kwa lengo la kushinikiza mkopaji kulipa kiasi kisichostahili, wakopaji kupewa mkopo pungufu kinyume cha makubaliano ya awali na kuwapo raia wa China wanaotumia teknolojia kutoa mikopo hiyo.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*



Wananchi wakipita kwenye Barabara ya King'azi, iliyoharibiwa kwa mvua na kuhitaji ukarabati katika Kata ya Kwembe, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# CCM wapeana tahadhari

**Na Waandishi Wetu**

KAMPENI za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa zimeshika kasi kwa viongozi wa kitaifa na makada wa vyama vya siasa kusaka kura za wenyeviti wa vijiji, mitaa na wajumbe.

Kanda ya Ziwa, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimewatuma Katibu Mkuu wake, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi kufungua kampeni Mwanza, Ally Hapi (Kagera), Hussein Bashe (Shinyanga), Issa Gavu (Geita) na Dk. Doto Biteko (Mara).

Mkoani Mwanza, Balozi Dk. Nchimbi alihimiza wanachama na viongozi kutambua mtaji wa imani walionao kwa watanzania na wazingatie mambo manne kuibuka washindi katika uchaguzi huo.

Aliwataka kukomaa na kampeni za nyumba kwa nyumba, mtu kwa mtu. Kuomba kura kwa wanachama na viongozi wa upinzani ili wawaunge mkono.

Mkoani Kagera, Katibu wa Jumuiya ya Wazazi CCM Taifa, Ally Hapi aliwataka wananchi kuchagua viongozi ambao watawasaidia katika kuwaletea maendeleo na kutatua matatizo yaliyoko katika maeneo yao.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa Kagera, Nazri Karamagi alisema mkoa huo una kata 192, vijiji 662, mitaa 66 na vitongoji 3,662, hivyo kutaka umoja katika kuhakikisha chama hicho kinachukua nafasi zote.

Katibu wa Halmashauri Kuu (NEC) Oganaizesheni na Mjumbe wa Kamati Kuu, Issa Gavu, akizindua kampeni hizo mkoani Geita, alisema wananchi wanatakiwa kukichagua chama hicho ili kusukuma maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

Naibu Katibu Mkuu wa CCM Bara, John Mongella, aliwataka wafuasi wa chama hicho kutofurahia migogoro inayofukuta ndani ya vyama vya upinzani au kusambaratika kwa vyama hivyo, akisisitiza kuwa vyama hivyo ni muhimu kwa maendeleo ya taifa.

Alitoa kauli hiyo juzi jijini Mbeya alipokuwa akizindua kampeni hizo kimkoa, akisema vyama vya upinzani ni muhimu katika kukuza demokrasia ya nchi.

Alisema agizo hilo ni sehemu ya utekelezaji wa 4R zilizoasisiwa na Rais Samia Suluhu Hassan ambazo lengo lake ni kulifanya taifa kuwa na utulivu ili maendeleo yapatikane kwa haraka.

**CHADEMA**

Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Victoria, Ezekia Wenje akizinduzi kampeni jijini Mwanza, aliahidi kuwa chama hicho hakitokata tamaa licha ya wagombea wake kuenguliwa katika kinyang'anyiro.

"Lengo ni kutufanya tukate tamaa lakini kwa kipindi hiki hatukati tamaa, bali tunaendelea mpaka kieleweke na kwa wale ambao wanashawishiwa waendelee kuweka msimamo kwani hii ni kazi ya kitume," amesema Wenje.

Mwenyekiti wa BAVICHA, Taifa John Pambalu alizinduzi kampeni hizo katika Kata ya Mahina, Butimba, Igogo na Mabatini jijini, aliwataka wananchi kushiriki kikamilifu katika upigaji kura utakaofanyika Novemba 27, 2024.

**AAFP, NLD**

Chama cha Wakulima (AAFP) kimesema kitanadi sera zake kwa kuwafikia wananchi nyumba kwa nyumba na kuwahamasisha kujitokeza kwa wingi kwenda kuwapigia kura viongozi wanaowataka.

Naibu Katibu Mkuu Taifa Maik Mhomela, alisema jana kuwa wanaamini kampeni hizo zitawafikia hata wale wasiotaka kwenda kusikiliza kwenye mikutano ya hadhara.

Chama cha The Nation League for Democracy (NLD), kilizindua kampeni zake jana kikitamba kitasaidia kutanua wigo wa ajira na maendeleo nchini, na kulaani vikali serikali kuwatumikisha kazi ngumu, ikiwamo kuchimba mitaro, visima na mabwawa wananchi waliomo katika programu za kupunguza umasikini nchini.

Uzinduzi wa kampeni zake zimefanyika katika Kijijij cha Kwedikwazu wilayani Handeni, mkoani Tanga ambako Katibu Mkuu wa NLD, Doyo Hassan Doyo alisema, "Kijiji hiki tumesimamisha wagombea. Kijiji hiki kina madini lakini kwenye akaunti ya kijiji hakuna hata mia mbovu, mana yake uongozi uliokuwapo madarakani umeshindwa kusimamia maslahi ya wakazi wa kijiji hiki."

**ACT WAZALENDO**

Kiongozi mstaafu wa ACT Wazalendo, Zitto Kabwe, aliwataka wananchi wa kijiji cha Ilalanguru, Jimbo la Kigoma Kusini, mkoani Kigoma kuchagua viongozi wanaowajibika.

Akihutubia wananchi katika mkutano wa hadhara jana, Zitto alisema kwenye maeneo ambayo wagombea wa vyama vya upinzani wameenguliwa na kubakia wa CCM, wawapigie kura ya 'HAPANA'.

"Miaka mitano iliyopita, uchaguzi kama huu tunaoifanya ulivurugwa, watu wakapitishwa bila kupingwa, wakatangazwa kuongoza vijiji na mitaa yetu bila ridhaa yenu.

"Mwaka huu figisu zipo, watu wameenguliwa lakini hakuna aliyetangazwa kupita bila kupingwa kwasababu chama chenu cha ACT Wazalendo kilichukua hatua muhimu sana," alisema.

Katibu wa NEC Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Amos Makalla, alisema jijini Dar es Salaam kuwa watakaoshinda kwa haki katika uchaguzi huo watatangazwa.

"Uchaguzi huu tunakwenda kupata viongozi tunaokwenda kuishi nao kila siku. Uchaguzi huu ni muhimu ili Rais Samia Suluhu Hassan akileta fedha za zahanati, viongozi hawa ndio wanaohusika.

"Lazima mwangalie ni aina gani ya wagombea ambao tukiwachagua watakuwa suluhisho la matatizo yetu na tutashirikiana nao. Tumewaletea wagombea wazuri watatuzi wa kero zetu," alisisitiza.

***SOMA ZAIDI Uk. 3**

***Imeandikwa na Vitus Audax, Rose Jacob (MWANZA), Marco Maduhu (SHINYANGA), Restuta Damian (KAGERA), Alphonce Kabilondo (GEITA), Paul Mabeja, Peter Mkwavila, Renatha Msungu (DODOMA),Elisante John (SINGIDA), Boniface Gideon (HANDENI), Nebart Msokwa (Mbeya), Restuta James na Romana Mallya (DAR) na Mussa Mwangoka (KATAVI).**

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# Tundu Lissu aibuka kisera zaidi

**Na Vitus Audax**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chadema, Tundu Lissu ameibuka na hoja mpya, safari hii akijikita kisera zaidi akiwataka wanachama na watanzania kutokuwa wanyonge kutokana na wagombea wao walioenguliwa katika kinyang'anyiro cha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Amesema wana nafasi ya kuwakataa katika sanduku la kura kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi huo kisha kurudiwa uchaguzi kwa kuwekwa wagombea wengine.

Alitoa kauli hiyo jana wakati akihutubia wananchi wa Nyamongo, huko Tarime Vijijini, mkoani Mara wakati wa ufunguzi wa kampeni za uchaguzi zinazoendelea katika maeneo mbalimbali nchini.

Lissu alisema chama hicho kina wagombea 2,612 nchi nzima na kuwa idadi hiyo siyo haba, hivyo kuwataka wananchi na wanachama wao kuhakikisha wagombea hao wanashinda, ikiwa ni sehemu ya kupunguza alichokiita "maumivu ya wale walioondolewa katika uchaguzi huo".

Alisema katika eneo la Nyangoto, kama ilivyo kwa maeneo mengine, mgombea wao wa nafasi ya mwenyekiti ameenguliwa katika kinyang'anyiro, hivyo kuwapatia kazi mbili wananchi wa maeneo yenye tatizo la namna hiyo ili kuhakikisha wanapata viongozi wanaowapenda baada ya walioteuliwa kuenguliwa.

"Kwanza, ni kuhakikisha wale wote waliobaki katika kinyang'anyiro washinda nafasi wanazozigombea. Mfano, katika eneo hili mkihakikisha tuna wawakilishi hawa 25 katika Halmashauri ya Kijiji, sisi ndiyo wenye uamuzi bila kujali kiongozi ni yupi," alisema Lissu.

Alitaja mbinu nyingine ya kuwakataa wagombea aliodai "wamewekwa bila idhini ya wananchi", ni kuwapigia kura ya 'HAPANA' na kuwa kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi, ili mgombea ashinde nafasi hiyo ni lazima awe na kura za ndio zaidi ya asilimia 50.

"Hii ni tofauti na kanuni za mwaka 2019, tukishapiga kura za 'HAPANA' kwa namna yoyote, lazima mwezi ujao turudie uchaguzi na sisi tutaweka wagombea wetu, na ninajua mtafanya mnachokifanya miaka yote, hamtakubali kuibiwa kura, atakayejaribu kutuchezea kwenye kura, mnajua cha kumfanya, hivyo ninajua tutashinda kwa kishindo," alisema Lissu.

Akiwa Lamadi, mkoani Simiyu, Lissu alisema nchi haitakombolewa kwa kupiga magoti na kufanya maombi, bali kwa kufanya mabadiliko ya msingi kwenye mfumo ya kuiendesha.

"Kwenye uchaguzi huu, si mnafahamu ambavyo wameharibu? Wameharibu sana, si tu kwa sababu ni wabaya bali pi kwa sababu hatukufanya mabadiliko ya msingi kwenye mfumo wetu wa kuendesha nchi.

"Wanaotengeneza kanuni za uchaguzi ni wao wenyewe, wanaozisimamia, wanaoamua mchezo uchezwe, marefarii na wachezaji ni wao wenyewe, unategemea nini? Unategemea tutendewe haki? Kama tusipopambana katika huu mwaka uliobaki, tukabadilisha sheria za uchaguzi, tukabadilisha na tume, mwaka ujao yatakuwa yaleyale.

"Nani anayeamini kwamba hawa wanaweza wakafanya tofauti na walivyofanya mwaka 2019 na mwaka 2020? Kwa hiyo, kwa huu mwaka mmoja uliobaki, tuache mchezo, tuache kuwachekea watatumaliza.

"Mwaka ujao yatakuwa ni yaleyale na yakitokea yaleyale, wajinga watakuwa ni sisi kwa sababu hakuna asiyeyajua wanayoyafanya, tukiruhusu wafanye tena, wajinga watakuwa sisi na hakuna visingizio.

"Nchi haikombolewi kwa maombi, haikombolewi kwa kupiga magoti kwa kumwomba Mungu, inakombolewa kwa mapambano, fanyeni kampeni, mkafanye uchaguzi, wagombea waweke ni kwenye nafasi tuanze kujijenga upya," alisema Lissu.

Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Shinyanga, Emmanuel Ntobi, aliwaomba wananchi kuchagua wagombea wanaotokana na chama hicho, kwa kuwa kina wagombea makini ambao wana maslahi na maisha ya wananchi.

"CHADEMA tumesimama imara kuhakikisha kila mwananchi anapata haki yake. Tunasimamia sera ambazo zitahakikisha huduma bora kwa wananchi wetu, bila kubagua mtu yeyote. Tutahakikisha miundombinu ya afya, barabara, elimu na huduma za jamii zinaboreshwa," alisema Ntobi.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA Taifa, Yahaya Alawi kutoka Zanzibar, akizindua kampeni mkoani Geita, aliwataka wananchi kufanya mabadiliko katika uchaguzi huo ili yawasaidie kunufaika na rasilimali za madini walizonazo mkoani humo.

Alisema madini ya dhahabu popote duniani ni hazina lakini wakazi wa eneo husika, yaani mkoa wa Geita, licha ya kujaliwa kuwa na utajiri wa rasilimali hiyo, wanakabiliwa na umasikini.

"Tufanye mabadiliko kwa kutumia haki ya kikatiba kupiga kura na kuwachagua viongozi wanaotokana na CHADEMA, jitokezeni kwa wingi Novemba 27, 2024 kutekeleza haki yenu hii ya msingi," alisema Yahaya.

***Imeandaliwa na Elizabeth Zaya (DAR), Vitus Audax, Marco Maduhu (SHINYANGA), Alphonce Kabilondo (GEITA).**

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*





Skani hapa kutembelea chaneli yetu



## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA FEDHA

## MWALIKO WA KUSHIRIKI MKUTANO WA PILI WA JUMUIYA YA WAHASIBU WAKUU WA SERIKALI AFRIKA-AAAG

Tanzania inatarajia kuwa mwenyeji wa Mkutano Mkuu wa Wahasibu wa Serikali wa Afrika mwaka 2024 (AAAG) utakaofanyika jijini Arusha kuanzia tarehe 2 hadi 5 Desemba, 2024.

Mkutano wa pili wa Jumuiya ya Wahasibu Wakuu wa Serikali Afrika utakuwa na mada mtambuka ambazo zitasaidia watumishi wa kada mbalimbali kuwaongezea ujuzi na Maarifa.

Pia Mkutano huu utasaidia Viongozi na Watumishi wa Tanzania kupata nafasi ya kubadilishana uzoefu na kupeana fursa na Viongozi na Watumishi toka nchi nyingine za Afrika, Benki ya Dunia na IMF. Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ada ya ushiriki ya mkutano ni **Shilingi za Kitanzania 1,300,000/=** kwa kila mshiriki. Hivyo, Mamlaka husika zinaombwa kuwaruhusu na kuwalipia Wahasibu, Wakaguzi wa Ndani, Maafisa Usimamizi wa Fedha, Maafisa TEHAMA na watumishi wa kada nyingine kuhudhuria mkutano huu.

Washiriki wote wanatakiwa kuanza kijisajili kupitia lango (portal) lifuatalo: https://conference.aaag.org.zm kuanzia sasa hadi tarehe 01 Disemba, 2024 na ada ya ushiriki ilipwe kupitia **akaunti namba 9924915301 yenye jina African Association of Accountants General (AAAG).**

Aidha, kwa Taasisi za Umma, Kampuni mbalimbali na watu binafsi wanaotaka kudhamini Mkutano huu kwa lengo la kujitangaza kibiashara na kufanikisha Mkutano huu; Wizara ya Fedha inawakaribisha.

Kwa mawasiliano zaidi piga Namba ya simu +255 713 525 592 barua pepe, veronica.kishala@hazina.go.tz na evans.sayile@hazina.go.tz Sanduku la Posta ni Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha S.L.P 2802, Dodoma.

Pia kama muombaji amesahau namba ya simu, barua pepe na Sanduku la Posta anaweza kupata mawasiliano kupitia wakuu wa Hazina Ndogo waliopo kila mkoa Tanzania bara na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali Zanzibar.

**Kwa Nakala Ngumu tafadhali wasilisha kwa anuani ifuatayo:**

**Sekretariati ya Kamati ya Maandalizi Mkutano wa AAAG,**
**Wizara ya Fedha**
**Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali**
**Jengo la Hazina (Ghorofa ya Pili),**
**18 Barabara ya Jakaya Kikwete,**
**S.L.P 2802,**
**DODOMA.**

**Tangazo hili limetolewa na:**

**KATIBU MKUU - HAZINA**
**Novemba, 2024**

# Ubomoaji jengo lililoporomoka Kariakoo waanza, kamati ya uchunguzi yazinduliwa

**Na Halfani Chusi**

UBOMOAJI wa jengo lililoporomoka Jumamosi Kariakoo, jijini Dar es Salaam na kusababisha vifo vya watu 20 na makumi wengine kujeruhi umeanza, huku Waziri Mkuu akizindua kamati ya uchunguzi wa tukio hilo na usalama wa majengo katika eneo hilo la kibiashara.

Juzi Rais Samia Suluhu Hassan alitembelea eneo hilo muda mfupi baada ya kuwasili nchini akitokea Brazil na kuagiza maduka yaliyoko mbali na eneo la tukio kuanzia jana yafunguliwe huku shughuli ya kulibomoa jengo na kuhifadhi mizigo ya wafanyabiashara ikiendelea.

Shughuli hiyo inafanywa na vyombo vya dola ambao hadi jana saa 11 jioni ilikuwa inaendelea huku mitambo mbali ikionekana ikitumika kunasua mizigo.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila alizungumza na Nipashe, akifafanua kuwa hatua inayofuata ni kuhifadhi mizigo iliyonasuliwa ili baadaye itambuliwe na wenye mali.

Alipoulizwa iwapo kuna watu wengine wameokolewa, Chalamila alisema hakuna mwili wala majeruhi wengine walioopatikana katika hatua hiyo.

"Wenye maduka wameunda kundi la WhatsApp, wanawasiliana kwa ajili ya kupeana taarifa kuhusu mizigo yao ambayo tutaihifadhi mahali salama kisha baadaye watakuja kuichukua.

"Unajua mizigo ikiangukiwa na jengo haiwezi kuwa sawa, kama ambavyo namna ghorofa hilo lilivyoporomoka, lakini zoezi la uhamishaji mizigo kupitia vyombo vya dola linaendelea na linakwenda vizuri," alisema Chalamila.

**KAMATI YAZINDULIWA**

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa jana alizindua Kamati ya Wataalamu ya Uchunguzi wa Jengo hilo na kuitaka ihakikishe kuwa inafanya uchunguzi kwa uwazi, haki na kwa kuzingatia viwango vya kitaaluma.

Alizindua kamati hiyo kwenye ukumbi wa mikutano ulioko Ofisi Ndogo ya Waziri Mkuu, Magogoni, jijini Dar es Salaam, akiagiza itekeleze majukumu yake kwa kufuata sheria, kanuni na maadili ya kazi.

Amesema mbali na kuchunguza jengo hilo lililoporomoka, kamati hiyo pia imeundwa ili kuchunguza majengo mengine yanayoendelea kutumika katika eneo la Kariakoo, kuchunguza uimara wa majengo yanayojengwa, kuchunguza endapo taratibu zinafuatwa wakati wa ujenzi, ikiwamo vibali, makandarasi wenye sifa na usimamizi wa mamlaka husika wakati wa ujenzi.

Waziri Mkuu alisema madhumuni mengine ya kuundwa kwa kamati hiyo ni pamoja na kuchunguza endapo ubore-shaji majengo unaofanywa Kariakoo unazingatia sheria, kanuni na taratibu pamoja na kubainisha majengo yote yaliyo katika hatari ya kuanguka na kupendekeza hatua za kuchukua.

Tarehe 16 Novemba mwaka huu, saa tatu asubuhi, ilitokea ajali ya kuporomoka kwa jengo la ghorofa tatu katika Mtaa wa Agrey, kata ya Kariakoo, jijini Dar es Salaam na kusababisha athari kubwa kwa watu na mali katika eneo hilo. Baada ya ajali hiyo, Rais Samia alimwelekeza Waziri Mkuu kuunda kamati hiyo ya uchunguzi.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza na Kamati ya Wataalamu wa Uchunguzi wa Jengo lililoporomoka eneo la Kariakoo, baada ya kuizindua, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OWM**

## Apandishwa kizimbani kwa mashtaka kunyonga mtoto

**Na Grace Gurisha**

AMINA Ally (21), mkazi wa Kigogo, Dar es Salaam amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Wilaya ya Kinondoni, akikabiliwa na mashtaka ya kumnyonga mtoto wake mwenye umri wa siku moja na kusababisha kifo chake.

Mshtakiwa huyo amepelekwa mahabusu baada ya kushindwa kutimiza masharti ya dhamana ya kuwa na mdhamini mmoja ambaye ni mtumishi wa serikali aliyetakiwa kutia saini bondi ya Sh. milioni 10.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali Sada Mohamed alidai juzi mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Is-haq Kupa kuwa mshtakiwa anatuhumiwa kuangamiza kichanga chini ya kifungu cha 199 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura 16, kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

Alidai kuwa mshtakiwa ambaye kazi yake ni mkulima, anatuhumiwa kuwa Oktoba 27, 2024, akiwa eneo la Kigogo ndani ya wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam, kwa hiari alimnyonga mtoto wake wa kiume wa siku moja na hivyo kusababisha kifo chake.

Baada ya kusomewa shtaka hilo, alikana kuhusika na tuhuma hizo kwa sauti ya chini, Hakimu Kupa alimweleza kwamba hatakiwi kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza shauri hilo.

Hakimu Kupa alimwuliza Wakili Mohamed kama shtaka hilo lina dhamana au la; naye alidai lina dhamana kwa mujibu wa sheria.

"Ili uwe nje kwa dhamana unatakiwa uwe na mdhamini mmoja ambaye ni mtumishi wa serikali, tutakwenda kuangalia ofisi yake, atatia saini bondi ya Sh. milioni 10," alisema Hakimu Kupa. Mshtakiwa alidai kuwa hana wadhamini, Hakimu Kupa akamweleza kwamba anaahirisha kesi hiyo hadi Desemba 5, 2024, lakini siku yoyote akipata wadhamini karatasi ya kumtoa gerezani itatolewa na atapelekwa mahakamani kisha atadhaminiwa.

"Hata ukipata kesho wadhamini, karatasi ya kukutoa gerezani ipo itatolewa, ukiwapata waeleze masharti ya dhamana waje kukudhamini," alisema Hakimu Kupa.

# 12 kutoa ushahidi kesi ya kutishia kwa bastola

**Na Grace Gurisha**

MASHAHIDI 12 na vielelezo saba vinatarajiwa kutumika katika kesi ya tuhuma za kujeruhi inayomkabili Derick Junior (36), ambayo kipande cha picha jongefu (video) kilichosambaa katika mitandao ya kijamii kinaonesha akimshambulia na kumjeruhi Julian Bujulu kwa kitako cha bastola.

Aidha, Junior amekanusha kumiliki bastola licha ya alikubali kujisalimisha polisi na pia amekataa kutoa silaha hadharani katika tukio lililotokea eneo la Masaki katika Klabu ya 1245, wilayani Kinondoni.

Taarifa hiyo imetolewa juzi na Wakili wa Serikali, Sada Mohamed mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Is-haq Kupa wa Mahakama ya Wilaya Kinondoni, Dar es Salaam, baada ya kumaliza kumsomea mshtakiwa maelezo ya awali (PH).

"Tutakuwa na mashahidi 12 na vielelezo saba tayari nimeshawapa maelezo ya mlalamikaji, tunaomba tarehe kwa ajili ya kuanza kusikiliza mashahidi," alidai Mohamed.

Hata hivyo, Wakili wa mshtakiwa Jeremiah Mtobesya alidai kuwa wamepokea taarifa hiyo na kuhusu ushahidi na vielelezo kwa upande wao watazungumzia kipindi watakapofungua utetezi wao.

Awali, Mohamed wakati anasoma maelezo hayo mshtakiwa alikubali taarifa zake binafsi na pia alikiri kujisalimisha kituo cha polisi.

Hata hivyo, alikanusha kuwapo klabu na mlalamikaji (Bujulu) na kwamba hakukuwa na majibizano baina yao wakiwa katika eneo hilo.

Pia, Junior alikanusha kuwa video iliyozunguka mtandaoni sio yeye na hakumpiga usoni Bujulu eneo la jicho hadi kuvuja damu. Mohamed akiendelea kumsomea, Junior alikanusha Bujulu kupelekwa hospitali na pia hakuhojiwa na wala hakumpiga.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Januari 21, 2025, kwa ajili ya kuanza kusikilizwa kwa mashahidi wa upande wa Jamhuri, dhamana ya mshtakiwa inaendelea. Derick, mkazi wa Salasala jijini Dar es Salaam alipandishwa kizimbani na kusomewa mashtaka mawili kuhusu tukio hilo.

Katika shtaka la kwanza linalomkabili ni la kujeruhi na shtaka la pili ni la kutembea na silaha hadharani kwa namna ya kuleta tishio kwa mtu.Inadaiwa mshtakiwa huyo alitenda makosa hayo Oktoba 27, saa 12.30 asubuhi, eneo la Masaki katika Klabu ya 1245, wilayani Kinondoni. Ilidaiwa siku ya tukio mshtakiwa alimjeruhi Julian Bujuru kwa kumpiga kwa kitako cha bastola na kumjeruhi usoni (sehemu ya jicho na puani).

Inadaiwa katika eneo hilo la klabu hiyo, mshtakiwa alitoa silaha na kumtishia Bujuru, kitendo ambacho kinatishia amani kinyume na kifungu cha 84 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu.

Baada ya kusomewa mashtaka yake mshtakiwa huyo alikana kutenda kosa hilo. Mshtakiwa alitimiza masharti ya dhamana ya kuwa na mdhamini mmoja anayetambulika kisheria aliyetia saini bondi ya Shilingi milioni nane.

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***

**TANGAZO**

**PUBLIC NOTICE**

NSSF — We Build Your Future

# EXTENSION OF TIME BY TWO WEEKS FROM 23RD NOVEMBER TO 06TH DECEMBER 2024 TO ALLOW SUBMISSIONS FOR EXPRESSION OF INTEREST (EOI) TO INVEST IN FUND'S LANDS

The National Social Security Fund (NSSF) is established under the National Social Security Fund Act Cap 50 R.E. 2018 having its Head office located at Benjamin William Mkapa Towers, Azikiwe Street,Dares Salaam.

1.0 The Fund owns parcels of land in prime areas in various regions in Tanzania which can be developed into residential, commercial, industrial and other mixed commercial uses.

2.0 As part of its investment strategy, the Fund is planning to develop some of these parcels of land through a Joint Venture arrangement in a form to be agreed upon between the Fund and the Investor or a Long-Term Lease.

3.0 The parcel of land earmarked for development through anyof the above-mentioned arrangements are as tabulated hereunder:

| SN. | LAND DESCRIPTION | REGION | SIZE ($M^2$) | *CURRENT LAND USE | LAND ATTRIBUTES |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Plot No.1 & 2 Block D Kunduchi Beach,Kinondoni Municipality | DSM | 25,036 & 37,691 | Hotel | The plots are located at the Kunduchi beach area, about 1.5 km from the junction of Kunduchi Road and Ununio Road.Plots face the Indian ocean and the notable landmark is Wet &Wild Water Park |
| 2 | PlotNo.40& 41- Bahari Beach, Kinondoni Municipality | DSM | 4,888 & 5,553 | Residential | Plots are located along BahariBeach Street, about 200m from the junction of Ununio Road and Bahari Beach Road. A notable landmark is the Budget Resort |
| 9 | Plot No. 284-294,296,298,30 0 & 302 Block LL, Lubaga | Shinyanga | 2234 | Residential | The plots are located in the newly developed residential area of Lubaga Joshoni area about 0.8 km from Shinyanga - Mwanza Road<br>The neighbourhood is characterized with residential plots changing to institutional and commercial uses |
| 10 | Plot No.2 Block A Ligula Road,Mtwara Municipality TANU Road,Mtwara | Mtwara | 4,280 | Residential | The Plot is located along Ligula Road in a residential and commercial neighbourhood about 500m from Mtwara Central Business District |
| 11 | Plot No.14- 21 & 37-41 Block I, TANU Road,Mtwara Municipality | Mtwara | 5,740 | Office | Plots are located along TANU Road adjacent to TICL offices Mtwara Branch and Cashewnut Board. The Neighbourhood is mainly residential, institutional and commercial buildings |
| 12 | Farm No.18168 Mtawanya,Mtwara District Council | Mtwara | 2,100,320 | Agriculture | The farm is located at ZiwaniVillage about 15km from Mtwara town center. A notable landmark is Mtawanya Water Pumping Station |
| 13 | Farm No 71, Ziwani area,Mtwara District Council | Mtwara | 1,009,000 | Agriculture | The farm is located at Ziwani Village, Mtwara Mikindani about 23km from Mtwara town centre |
| 14 | Mmongo Beach Plots (31 plots), LindiTown Council | Lindi | 90,877 | Residential, Hotel, Commercial and Housing Estates | The plots are located about 11km from Lindi town and about 2 km from Lindi - DSM Road. A notable landmark is the Resident Magistrate Court of LindiRegion |
| 15 | Mabano Beach plots (245 plots), LindiTown Council | Lindi | 220,255 | Residential, Hotel, Commercial and Housing Estates | The plots are located about 13km from Linditown and about 2 km from Lindi -Dares Salaam Road |
| 16 | Plots No.122 -131, Njiro Hill,Arusha City Council | Arusha | 4,440 | Residential | Plots are located about 15 km from the Arusha city center and are accessed via Faru Street which branches off Njiro road at"Njiro kwa Masister" |
| 17 | Plot No.249 Block D, Njiro Area,Arusha City Council | Arusha | 39,610 | Residential | The property is located at Njiro area near Ebenezer Retreat Lodge. The plot was formerly owned by the Mukidoma School |

*The current use can be changed depending on the submitted concept and upon obtaining approval from relevant authorities

4.0 The Fund is seeking eligible,competent,and reputable investment Partner(s) who demonstrate the appropriate capabilities, expertise, and experience to invest in developing the above-mentioned parcels of land

5.0 The Fund invites sealed submissions for expression of interest from eligible and reputable local and international investors to formally express their interest in becoming preferred investors in developing the parcels of land through a Joint Venture or Long-Term Lease arrangement. Interested and eligible investors must provide the following information:

5.1 Application letter;
5.2 A Bankable Business Plan/ feasibility study;
5.3 Project proposal;
5.4 Concept Design;
5.5 Cost estimates;
5.6 Preferred financing arrangement;
5.7 Company Profile;
5.8 Company registration documents;
5.9 Audited and Financial statement for the past three years;and
5.10 Proposed Lease Terms in case of Long-Term Lease

6.0 The submitted financing arrangement must be accompanied by proof of availability of funds for the proposed project in the form of a bank statement or line of credit from a reputable financial institution or any other evidence

7.0 Interested eligible local and international investors may submit their expression of interest as a company or as a consortium of two or more companies

8.0 The companylies expressing interest can be local or foreign,upon successful award in the case of foreign investors, they will be obliged to be registered by TIC and other legal relevant authorities

9.0 Five years(5) experience in Sub-Saharan Africa in the proposed investment will be an added advantage

10.0 Potential investors shall not engage in any instance of inside dealing and should be free of any conflict of interest;

11.0 The potential investors who wish to physically visit the parcels of land may do so from 23rd November to 06th December 2024 through the following contacts:
i. Dar es Salaam Plots: Contact person: Estates Management Manager,Mr. Geofrey A.Timoth,Tel No.0753567260;
ii. Bagamoyo Farm: Contact person: NSSF Coast Regional Manager, Ms. Witness Patrick,Tel No.0746238415;
iii. Geita Plots: Contact person: NSSF Geita Regional Manager, Ms.Winnie Lusingu,Tel No.0746260794;
iv. Shinyanga Plots:Contact person NSSF Shinyanga Regional Manager, Ms. Amina Mdabi,Tel No.0767140926;
v. Mtwara Plots and Farms:Contact person:NSSF Mtwara Regional Manager, Mr.Rebule Maila Tel No.0756140358;
vi. Arusha Plots: Contact person: NSSF Arusha Regional Manager, Mr. Josephat Komba Tel No.0756140182;and
vii. Lindi Plots: Contact person: NSSF Lindi Regional Manager, Mr. Juma Namuna Tel No.0758803091.

12.0 Interested investors may seek clarification in writing and the same to be received at least seven(7) working days before the date of closing the Expression of Interest

13.0 The Fund reserves the right to accept or reject any submission and to annul the expression of interest process and reject all submissions at any time prior to short-list and awarding, without thereby incurring any liability to the affected applicant

14.0 All applications should be submitted on or before 4:00pm on **06th December 2024.**

Further, application should be directly addressed and submitted to the Director General through the following modes:

1. **Postal address :** Director General
National Social Security Fund,
P.O.Box 1322,
Dares Salaam,Tanzania

2. **Email address :** dg@nssf.go.tz

3. **Physical address** : NSSF Headquarters,
BenjaminiW.Mkapa Towers,17th floor, Azikiwe Street,Dares salaam

**Issued by:**
**Public Relations & Members Education Unit**

@NssfTanzania | www.nssf.go.tz

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kampeni ziwe za kistaarabu, kashfa matusi viepukwe

**KAMPENI** za uchaguzi wa Serikali za Mitaa, zimeanza rasmi juzi nchini kwa vyama vyote vya siasa vilivyojitosa kwenye uchaguzi huo kunadi wagombea wao. Kikubwa wananchi wanachotaka kukisikia kwenye kampeni hizo ni sera za vyama na viongozi watakaochaguliwa watakavyoweza kutatua kero zao.

Kampeni za kashfa, matusi wananchi hawataki kuzisikia wanataka kusikia viongozi hao watawafanyia nini kuondoa malalamiko ya mara kwa mara kwenye mitaa yao.

Ahadi zitakazotolewa kwenye kampeni hizo ndizo wananchi zitakazowafanya wawachague wanaojinadi badala ya kusikiliza kashfa na matusi.

Katika uzinduzi wa kampeni hizo juzi, vyama mbali mbali vitakavyoshiriki kwenye uchaguzi huo vimejinadi kufanya kampeni za kistaarabu kwa kuepuka kejeli na matusi.

Akizindua kampeni za Chama cha Mapinduzi (CCM), Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa chama hicho, Amos Makalla, amewahakikishia wananchi kuwa chama chake ndio kinachoongoza na kwamba ajenda na hoja nyingi ni kuwashawishi wananchi wakichague.

Aliahidi kuwa chama kitasimamia falsafa ya R4 za Rais Samia Suluhu Hassan kwa kufanya kampeni hizo kistaarabu.

Viongozi watakaoshinda kwenye uchaguzi huo, wameonywa kutotanguliza maslahi yao mbele na kwamba chama kinaweza kuwaondoa katikati ya muhula wa uongozi.

Aidha, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimejinadi katika mikoa mbali mbali kupitia viongozi wake, akiwamo Tundu Lissu, Freeman Mbowe, John Mrema, Godbless Lema na Salum Mwalimu.

Viongozi hao wamejinasibu kuwa ushindi ni lazima kwa wagombea wao na lengo ni kuleta mabadiliko.

Chama cha ACT-Wazalendo nacho kilitawanyika katika maeneo mbali mbali kunadi wagombea wake kuanzia juzi.

Chama hicho kupitia Ofisa Habari wake, Abdallah Hamis, kilisema kuwa kiongozi wa chama hicho, Dorothy Semu, ataendesha kampeni mkoani Pwani wakati kiongozi mstaafu, Zitto Kabwe, atapiga kambi Kigoma.

Vyama vitatu tayari vimeanza kampeni hizo na kuweka ratiba ya mikoa itakayofanyika kampeni hizo.

Tunachotarajia ni kuona kampeni zinamalizika kwa amani mpaka siku ya kupiga kura, wananchi wachague wagombea wa vyama vilivyonadi sera zao vizuri na kueleweka.

Inapotokea vyama kwenda kinyume na lengo la kampeni, hapo ndipo dhana ya kunadi sera inapotea na kuingia kwenye siasa chafu za kuchafuana kwa matusi na kejeli.

Wananchi wamechoka kusikia matusi wanachotaka ni kuletewa maendeleo kwenye mitaa yao. Na hii inatokana na wengi wanaochaguliwa wanapoingia kwenye uongozi wanajisahau na ahadi zote walizotoa hazitekelezwi.

Wanachotaka wananchi ni kuona wanapowasilisha kero zao kwa viongozi waliowachagua wanazishughulikia na ikiwezekana kwa kushirikisha wananchi wa mitaa yao. Kwa sababu kila mtu anapoona kiongozi wake ana dhamira ya kuleta maendeleo lazima ataungwa mkono.

Kinachosubiriwa ni kuona matokeo ya kampeni hizo yanaleta mabadiliko kwa kuwajenga wagombea watakaopita kufanya vizuri kwenye uongozi.

Kura ndio mwamuzi wa mwisho, jinsi chama kitakavyonadi sera zake na wagombea wake ndivyo wananchi watakavyoshawishika kuchagua.

Vivyo hivyo, matokeo yatakapotangazwa ni matarajio yetu yatapokewa kwa amani na kama kuna pingamizi zitumike njia sahihi za kudai haki badala ya kudai kwa vurugu hali inayoweza kusababisha uvunjifu wa amani.

Uchaguzi huu wa Serikali za Mitaa ndio utakaoonyesha ukomavu wa Watanzania kuelekea Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwakani.

Mungu ubariki uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Tukielekea 'Upingaji Ukatili Jinsia', itukae vichwani, si vita lelemama

**KUNA** baadhi ya mikoa nchini imekuwa ikitajwa kuongoza kwa kukithiri vitendo vya ukatili wa kijinsia, hususani kuanzia ngazi ya familia. Hiyo ni kutokana na jamii kuamini kuwa iko ndani ya mila na utamaduni wa makabila ya huko.

Mbaya zaidi, jamii hizo zimekuwa zikichukulia kuwa ni jambo la kawaida na kuamua kufanya siri kwa kuhofia wahusika, kuangukia kwenye mikono ya dola na kuchangia kuendelea kukithiri kwa matukio hayo nchini.

Kukithiri itendo hivyo, sasa kumeziibua taasisi na mashirika yasiyo ya kiserikali nchini kupinga, baada ya kufanya utafiti na kubaini kuwapo jamii zisizo na elimu, kuhusiana na madhara ya vitendo hivyo. Wanaishia na hisia kwamba, hakuna haja ya kuyaripoti katika mamlaka husika.

Taasisi na mashirika hayo yamekuwa yakifanya kampeni hususani katika mikoa, ambako kumekithiri kwa vitendo hivyo, kwa lengo la kuwaelimisha wananchi madhara yake na umuhimu wa kuripoti kwenye vyombo vya dola mahali panakotokea matukio hayo.

Kampeni hizo zimesaidia kuibua matukio mengi ya aina hiyo na mengine yaliyokuwa yakifanyika katika jamii, ingawa bado kwa uchache yapo yanayoendelea.

Vitendo hivyo ni pamoja na watoto wadogo kubakwa, kulawatiwa na kwa wanafunzi mabinti kukatisha masomo kwa kupata ujauzito wakiwa shuleni, huku wazazi wakiachiwa jukumu la kulea wajukuu.

Wengine wamekuwa wakikumbana na ndoa za utotoni, baada ya kulazimishwa kuolewa kutokana na tamaa za wazazi kupata utajiri wa haraka mahari, huku wakisahau kufanya hivyo ni kuwaharibia msingi wa maisha yao baadaye na hata kisheria wanawajibika

**Wengine wamekuwa wakikumbana na ndoa za utotoni, baada ya kulazimishwa kuolewa kutokana na tamaa za wazazi kupata utajiri wa haraka mahari, huku wakisahau kufanya hivyo ni kuwaharibia msingi wa maisha yao baadaye na hata kisheria wanawajibika**

Hali hiyo imekuwa ikichangia vitendo hivyo kuendelea kusambaa katika maeneo mengine nchini na hata kwenye taasisi za elimu kama shuleni, vyuoni na sehemu kazi.

Hiyo ndio sababu ya viongozi wa taasisi, mashirika hayo na hata waliko serikalini, kupitia wizara husika, sasa wamesimama kidete kwa kuitaka jamii kubadilika na kuwafichua watu wanaojihusisha navyo.

Wakati ukanda wote wa dunia, ikiwamo Tanzania inaelekea kwenye Maandalizi ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia ambayo kila mwaka hufanyika kuanzia Novemba 25 hadi Desemba 10, jamii ibadilike na kuunga mkono jitihada hizo.

Jitihadha hizo zifanyike kwa kushiki kikamilifu katika kampeni za kuwafichua watu wanaojihusisha na vitendo hivyo, kwa sababu wanazidi kuharibu vizazi vya sasa na vijavyo.

Ushahidi unaonyesha kwamba, vitendo hivyo vinaendelea kuota mizizi katika jamii, kutokana na baadhi ya vizazi kurithi kwa kushuhudia vinafanyika kuanzia katika umri wao mdogo.

Mfano wa matukio hayo ni yale ya kutisha ya mauaji yanayoendelea kutokea katika jamii, yakiwamo ya wanandoa na watoto wadogo wasiokuwa na hatia.

Kwa kufanya hivyo, niseme tutakuwa tunaelekea kuwa na taifa ambazo litafanikiwa kutokomeza matukio ya ubakaji wanawake na watoto, vipigo ambavyo vimekuwa vikisababisha wanawake kuuawa na wenzi wao na rushwa ya ngono vyuoni na sehemu za kazi.

Wakati hayo yote yakiendelea, utafiti wa Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia Watoto (UNICEF), umebaini wasichana milioni 120 duniani walilazimishwa kufanya ngono bila ya ridhaa yao.

Nao wanawake na wasichana milioni 200 walifanyiwa hayo ya ukeketaji katika nchi 30 duniani, huku wasichana na wavulana milioni 246 wakikumbana na ukatili wa kijinsia wakiwa shuleni.

## HABARI KITAIFA




Daktari wa Mifugo kutoka Kitengo cha Kutumia Mbegu Bora cha Interchick, Dk. David Comalla (katikati), akitoa mafunzo kuhusu ufugaji kuku wenye tija, ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, magonjwa na kujikwamua kiuchumi kwa wafugaji takribani 20 katika kijiji cha Maguruwe, Kata ya Msimbu, Wilaya ya Kisarawe, mkoani Pwani juzi. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

KUCHOMA MKE KWA MAGUNIA YA MKAA...

# Mshtakiwa: Mahakama isipokee barua yangu kukiri kosa kwa DPP

**Na Grace Gurisha**

MFANYABIASHARA Khamis Luwongo (38) anayetuhumiwa kumuua mkewe Naomi Marijani kisha kuchoma moto mwili wake kwa kutumia magunia mawili ya mkaa, ameomba mahakama isipokee barua ya kukiri kosa hilo aliyomwandikia Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP).

Kukiwa na madai hayo, Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam imekubali daktari aliyemfanyia uchunguzi wa akili mshtakiwa, afike mahakamani aulizwe maswali ya dodoso na upande wa Jamhuri kwa kuwa ripoti ilionesha wakati anafanya tukio, hakuwa timamu kiakili.

Luwongo alidai hayo juzi mbele ya Jaji Hamidu Mwanga wa Mahakama hiyo wakati akiulizwa maswali ya dodoso na Wakili wa Serikali Mkuu Yasinta Peter aliyesaidiwa na Mwasiti Athuman, Ashura Mzava na Eric Kamala baada ya kumaliza kutoa utetezi wake.

Mshtakiwa aliulizwa maswali ya dodoso kwa nyakati tofauti na mawakili hao. Sehemu ya mahojiano hayo ni hii:

**Yasinta:** Mshtakiwa uliandika barua ya kukiri kosa kwa DPP?

**Luwongo:** Ni sahihi kabisa!

Yasinta: Uliandika barua hiyo ukiwa wapi?

**Luwongo:** Nikiwa Gereza la Segerea.

Yasinta: Hao askari uliosema walikutesa ili ukiri kosa, walikuwa nyuma yako wakati unaandika barua hiyo? Tupo hapa kwa ajili ya kutenda haki, si mbaya mahakama ikapokea kama kielelezo.

**Luwongo:** Sihitaji Jaji uione kabisa, sijui wameileta hii barua ya nini?

**Jaji:** Ili barua uifafanue, lazima ipokewe mahakamani, kwa sasa huwezi kuielezea ndiyo maana wanataka uitoe kwanza kama kielelezo.

**Yasinta:** Kwani Luwongo unaficha nini hapo kwenye barua?

**Luwongo:** Kiufupi, sioni msingi wowote wa hii barua kupokewa, sitaki kabisa ipokewe kama kielelezo.

**Yasinta:** Uliwahi kutoa statement (maelezo) mbele ya Hakimu Ruboroga na Rugemalira kwamba huogopi kunyongwa, lakini unyongwe kwa haki kwa sababu hukuua kwa kukusudia?

**Luwongo:** Sikumbuki.

**Yasinta:** Kwanini unapeleka lawama kwa watu wengine, hasa viongozi wa dini, kwamba na wao wamehusika na tukio hili kwani na wao walikuwapo?

**Luwongo:** Viongozi wa kanisa wanajua ugomvi wetu.

Yasinta: Mahakama ichukue jina gani kati ya Magreth na Janeth, kwa sababu ulisema siku ugomvi unatokea ulilala kwa Magreth, kwa sasa unasema Janeth?

**Luwongo:** Kiufupi, hapa ninazungumzia Magreth na siyo Janeth, nilikosea tu jina.

**Yasinta:** Katika ushahidi wako ulisema mke wako alikuvuta sehemu za siri hadi ukapata giza na ulipoamka hukumkuta, hebu ielezee mahakama kwa sababu hatukuwapo eneo la tukio, yeye alisimama wapi na wewe ulikuwa wapi?

**Luwongo:** Sikumbuki.

**Yasinta:** Na wewe siku hiyo ulikuwa umevaaje hadi kushikwa huko chini, kwa sababu umesema ulilala nje ndiyo kwanza umefika?

**Luwongo:** Sikumbuki.

Yasinta: Kama hukumbuki, mbona umesema mke wako alikuwa amevaa kanga mbili na nguo ya ndani, wewe ulionaje hiyo nguo ya ndani?

**Luwongo:** Hii stori ilikuwa si ya kweli, nimetunga tu.

**Yasinta:** Hebu shahidi tuambie, kwa hiyo ulivyomaliza kumpiga, ukajua hapa Naomi kafa ukaamua kumchoma?

**Luwongo:** Mimi mke wangu hajafariki (dunia), wewe ndiyo unithibitishie mahakama hapa bila kuacha shaka yoyote.

**Yasinta:** Unataka uthibitisho gani kwamba Naomi amekufa?

**Luwongo:** Ninahitaji uthibitisho wa kisayansi na Mkemia ameshindwa hata yeye kuthibitisha kifo chake.

**Yasinta:** Jinsi ulivyomchoma hadi majivu ulitegemea Mkemia alete nini?

**Luwongo:** Mimi sijamchoma mke wangu.

**Yasinta:** Kabla ya kukamatwa ulikuwa unateswa na askari polisi kama ulivyoeleza?

**Luwongo:** Ndio, nilikuwa ninateswa, ninarudi nyumbani nikiwa na maumivu sana, ninatumia dawa tena hadi waniachie ndugu zangu walikuwa wanatoa fedha kwa polisi ndiyo wananiachia.

**Mzava:** Ulikuwa unamaanisha nini kwamba ulijisikia giza?

**Luwongo:** Kiuhalisia mimi mwenyewe sijui.

**Mzava:** Ulishawahi kupelekwa Mirembe kwa ajili ya uchunguzi?

**Luwongo:** Ni kweli kabisa.

**Mzava:** Kwanini hukutumia ripoti ya majibu katika utetezi wako?

**Luwongo:** Taarifa zote zipo mahakamani.

Baada ya maswali hayo, ya dodoso, Wakili wa Mshtakiwa, Hilda Mushi alifunga utetezi wao na kueleza mahakama kwamba walikuwa na shahidi mmoja tu ambaye ni mshtakiwa peke yake.

Wakili Yasinta aliomba mahakama iwapatie Dk. Sadik Mandari aliyehusika kumchunguza Luwongo ili afike wamwulize maswali ya dodoso yatakayoweza kufikia mahakama kutenda haki kwa kuwa ripoti ipo kwenye mwenendo wa kesi. Wakili Hilda alidai kuwa hawana pingamizi na daktari huyo kuletwa mahakamani.

"Kwa kuwa daktari amemchunguza mshtakiwa na taarifa zikaletwa mahakamani kwamba mshtakiwa ana changamoto ya akili, kabla mahakama kupanga kuamua shauri hili tumpate aje, kwa hiyo nimekubali na upande wa utetezi watapata nafasi," alisema Jaji Mwanga.

Kesi iliahirishwa hadi Novemba 25, 2024 kwa ajili ya maswali ya dodoso na samansi zitolewe kwa mhusika. Mshtakiwa Luwonga ambaye ni mkazi wa Kigamboni, Dar es Salaam, anadaiwa Mei 15, 2019, akiwa Gezaulole, wilayani Kigamboni, alimuua Naomi Marijani.

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***

## 'EAC iweke mifumo ya teknolojia kudhibiti usafirishaji haramu wa mazao ya misitu'

**BAKU, Azerbaijan**

TANZANIA imetoa wito kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuunganisha mifumo ya teknolojia katika ufuatiliaji na usafirishaji mazao ya misitu ili kupunguza tatizo la uvunaji na usafirishaji haramu.

Pia inatarajia kushirikiana na wadau wa maendeleo, likiwamo Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) ili kuongeza juhudi katika upatikanaji rasilimali fedha na teknolojia za ufuatiliaji wa mazao ya misitu kuanzia kwenye maeneo yanakovunwa.

Wito huo ulitolewa jana na Mhifadhi Mkuu wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Dk. Elikana John wakati akiwasilisha mada katika mkutano wa pembezoni mwa Mkutano wa 29 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP29) unaofanyika Baku, Azerbaijan.

Mkutano huo unaangalia mchango wa sekta ya misitu kwenye kupunguza uzalishaji gesi joto katika ufuatiliaji na usimamizi endelevu wa misitu barani Afrika.

Ni mkutano huo uliandaliwa na Wizara ya Mazingira, Mabadiliko ya Tabianchi na Misitu (MECCF) ya Kenya, Wakala wa Misitu Kenya (KFS) na JICA.

Dk. Elikana aliwasilisha mada pamoja na wadau wa Afrika ya Mashiriki kuhusu matumizi ya teknolojia na mifumo ya kufuatilia usafirishaji mazao ya misitu unayofanywa na TFS ili kuendeleza uvunaji endelevu na kuimarisha uhifadhi wa misitu na kupunguza uvunaji haramu, pia kuongeza mapato ya serikali.

Mkutano huo umewaleta pamoja na kuwaunganisha wadau wa Afrika Mashariki, washirika wa maendeleo wakiongozwa na JICA katika kuchagiza na kujenga uelewa wa wadau na kuwezesha utaalamu na upatikanaji rasilimali fedha kwa wadau wa Afrika Mashariki.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**



# Liwale kuanzisha biashara hewa ukaa

**Na Ashton Balaigwa**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi ipo katika hatua ya kuanzisha biashara ya hewa ukaa kwenye misitu ya vijiji na halmashauri ili kuongeza mapato ya ndani ya mazao ya misitu ambayo kwa sasa tayari wameshakusanya Sh. bilioni 2.9 katika kipindi cha mwaka 2023 kutokana na uvunaji endelevu.

Mpango huo umekuja baada ya halmashauri hiyo kwenda kujifunza Wilaya ya Tanganyika, mkoani Katavi ambayo imekuwa mnufaika mkubwa wa mapato ya biashara ya hewa ukaa kwa kutumia misitu iliyohifadhiwa.Ofisa Maliasili na Mazingira wa wilaya hiyo, Deogratias Simwanza, aliwaambia waandishi wa habari wa Mazingira Tanzania (JET) wanaofuatilia utekelezaji wa mradi kupunguza migongano baina ya binadamu na wanyamapori unaotekelezwa na Shirika Maendeleo la Ujerumani (GIZ) kwa niaba ya serikali ya nchi hiyo.

"Pamoja na uvunaji endelevu na kupata fedha za rasilimali za misitu ya zaidi ya Shilingi bilioni mbili, tumeona kuna fursa nyingine ya kuongeza mapato kwenye biashara ya hewa ukaa na tayari tumepata mwezeshaji wa mradi huo na yupo katika hatua za kuanzisha biashara hiyo ili tuweze kunufaika," alisema Simwanza.

Alisema misitu katika wilaya hiyo ni moja ya chanzo kikubwa cha mapato kuanzia kwenye vijiji na halmashauri hiyo kutokana na kuhifadhiwa vizuri pamoja na usimamizi endelevu wa rasilimali hizo.

Alisema wilaya hiyo ina jumla ya vijiji 28 vyenye hifadhi ya misitu takribani 35 inayohifadhiwa na kufanyiwa uvunaji endelevu baada ya kufanya mpango wa usimamizi shirikishi wa misitu wa miaka mitano na mpango wa uvunaji endelevu wa misitu wa miaka mitano.

"Kimsingi hii misitu yote ni ya halmashauri ya wilaya, lakini yenyewe imekasimu majukumu ya usimamizi wa misitu katika vijiji na imefanyika ili kuongeza usimamizi zaidi na kupeleka manufaa kwa wananchi," alisema.

Kati ya makusanyo ya Sh. bilioni 2.5 zilizopatikana kwenye uvunaji endelevu wa misitu, Sh. milioni 500 ni mapato ya halmashauri ya wilaya hiyo na zilizobaki zimeingia kwenye vijiji kwaajili ya shughuli za maendeleo na usimamizi wa misitu.

Alisema kutokana na uvunaji endelevu unaofanywa, asilimia 50 ya mapato yanayopatikana yanabaki kwenye vijiji hivyo kwaajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo mbalimbali kwenye eneo hilo.

Alisema asilimia 30 mpaka 35 inabaki tena kwenye vijiji hivyo kwaajili wa shughuli za usimamizi wa misitu ikiwamo kufanya doria za kudhibiti uvunaji haramu ambayo imekuwa ikileta mafanikio na kuilinda misitu hiyo kwenye vijiji. Mkuu wa wilaya hiyo, Gudluck Mlinga, alisema wilaya hiyo inajivunia kuwa na hekta milioni mbili za uvunaji endelevu wa misitu ikiwamo ya miti ya mbao kutokana na uhifadhi mzuri unaofanywa.

Mlinga alisema wilaya hiyo inapata faida kubwa kutokana na uhifadhi wa misitu na aina nyingi ya miti, lakini kutokana na changamoto ya soko na mazoea, jamii inatumia aina mbili pekee ya miti ikiwamo mninga na mkongo na kwa uchache miti ya mtondoro.

"Wavunaji wakubwa wa misitu yetu ni Watanzania ambao ni wafanyabiashara wa mazao ya misitu na tunaendelea kushirikiana na wadau wengine kuongeza uelewa wa matumizi mengine ya miti iliyobaki kwakuwa tuna aina nyingi sana za miti ambayo inaweza kutumika kwaajili ya shughuli nyingine," alisema.



Baadhi ya wanachama wa Baraza la Wanawake la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA) mkoa wa kichama wa Ilala, Dar es Salaam, wakiwa katika kongamano la kuwajengea uwezo wagombea wanaojiandaa kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa, mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jafo ataja sababu bidhaa kukwama AGOA

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Selemani Jafo, amesema bidhaa nyingi za Tanzania zimeshindwa kuingia kwenye soko la Marekani, Sheria ya Ukuaji na Fursa Afrika (AGOA), kutokana na kushindwa kukidhi vigezo na masharti yaliyowekwa kwenye soko hilo.

Aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya utoaji wa tuzo za ubora kwa kampuni na wajasiriamali mbalimbali zilizoratibiwa na Shirika la Viwango (TBS).

Kwenye tuzo hizo TBS ilishirikiana na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (Tantrade), Chemba ya Wafanyabiashara Wanawake (TWCC), SIDO, Chemba ya wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA), Shirika la Viwango Zanzibar (ZBS) na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF).

Alisema Serikali ya Marekani ilitoa fursa hiyo kama mkakati wake wa kuzikuza nchi za Afrika, lakini baadhi ya nchi hizo ikiwamo Tanzania zimeshindwa kuuza bidhaa nyingi kwenye soko hilo.

Aliwataka wajasiriamali na wazalishaji nchini kuzalisha bidhaa zenye ubora ambazo zitaingia kwenye masoko makubwa ya kimataifa kama AGOA, Afrika Mashariki na kati na hata soko la ndani.

"Mataifa yote yaliyoendelea duniani huwa yanategemea soko la ndani kwanza sisi tuko milioni 62 kwa hiyo kama mtazalisha bidhaa ambazo Watanzania watazipenda soko la ndani tu linaweza kuwasaidia," alisema. Alisema tuzo hizo zimeonesha umuhimu mkubwa hasa kutokana na washiriki wake kuongezeka kutoka washiriki 36 wa mwaka jana hadi kufikia 54 wa mwaka huu.

"Kwa bara la Afrika TBS imekuwa mshindi wa taasisi za ubora barani Afrika kwa hiyo inatambulika kuwa namba moja kwa masuala ya udhibiti na tuzo zinasaidia sana kuongeza thamani ya bidhaa za kampuni na wajasiriamali wanaoshinda," alisema.

Aliwataka Watanzania kuwaunga mkono wenzao wanaozalisha bidhaa mbalimbali kwa kununua bidhaa hizo na kuachana na kasumba ya kuona bidhaa za nje kama bora zaidi ya zile zinazozalishwa ndani.

Aliwataka Watanzania kupitia Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo (SIDO), kuimarisha biashara zao kwa kupata mafunzo yanayotolewa na shirika hilo na baadaye kupewa nembo ya ubora bure na TBS.

Alisema idadi ya vijana wanaomaliza vyuo vikuu ni kubwa na serikali haina uwezo wa kuwaajiri wote hivyo kuna umuhimu wa kuendelea kuleta sekta binafsi ili iwaajiri vijana hao au wajiajiri wenyewe.

Mwenyekiti wa Kamati ya Tuzo hizo, Cresensia Mbunda, alisema kila mwaka Wizara ya Vianda na Biashara kupitia TBS na ZBS wakishirikiana na sekta binafsi wamekuwa wakiandaa tuzo za ubora.

Alisema wanafanya hivyo kama sehemu ya kuhamasisha matumizi ya viwango vya ubora na ushindani katika sekta mbalimbali nchini na kutambua na kuthamini juhudi za wazalishaji waliofanya vizuri kwa mwaka.

Alisema timu ya majaji saba kutoka sekta binafsi na serikali walipitia na kuchakataa maombi 52 yaliyokusanywa kwenye kuwania tuzo hizo bila upendeleo wowote na kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa.

# Tuzo Mwl. Nyerere kuondoa uhaba wa vitabu

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu, itasaidia kuondoa uhaba wa vitabu, kuchochea kasi ya usomaji na kuchangamsha soko la bidhaa hiyo nchini.

Akizungumza jana wakati wa hafla ya uzinduzi wa ugawaji wa vitabu vilivyoshinda tuzo hiyo, iliyofanyika juzi mkoani Dar es Salaam, Prof. Mkenda alisema wazo la kuanzisha Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ni mkakati maalumu wa kuchochea uandishi bunifu na kuondoa utegemezi wa vitabu vichache vilivyopo.

Alisema jukumu la kusimamia tuzo hizo lilikabidhiwa kwa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), ambayo inaratibu uandaaji wa vitabu mbalimbali vya wanafunzi, na kwamba hilo ni dirisha la kuhakikisha wanapata vitabu vingi ili kuwe na uwanda mpana wa kuchagua vitakavyotumika shuleni.

"Tunataka tuwe na waandishi wengi zaidi, hivyo TET muweze kuunda jopo kwamba hii tuzo iwe chanzo chenu cha kuwafikia waandishi kokote waliko kwasababu serikali itasaidia kuhakikisha kitabu kitakachoshinda kitanunuliwa na kusambazwa, na kusaidia kukuza Kiswahili ndani na nje ya nchi," alisema Prof. Mkenda.

Aliongeza kuwa miongoni mwa vitu wanavyovijadili muda mrefu ni ugumu uliopo katika sekta ya vitabu nchini ikiwamo kudorora kwa soko, na kwamba walielewa kuwa uwezekano wa kupata vitabu vizuri kwaajili ya kuendeleza utamaduni wa kusoma unazidi kuwa mgumu.

"Pia kulikuwa na hatari ya kampuni za uchapishaji kufungwa nchini, hivyo kati ya vitu ambavyo viliazimiwa ni kwamba serikali itafute namna ya kuchangamsha soko la vitabu kwa namna ambayo tunaweza kuweka bajeti ya kununua vitabu ambavyo tunavihitaji ili wachapishaji waone sababu ya kuchapisha vingi bila kuwa na wasiwasi wa soko.

"Hilo lilikuwa ni azimio la wadau wa vitabu, na kuanzisha Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya uandishi bunifu ili gurudumu la vitabu liendelee, niombe kuanzia leo tuepuke kuhusisha mtu binafsi na juhudi hizo kwasababu hili sio wazo la mtu mmoja linatokana na wadau wengi," amesema Prof. Mkenda.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Dk. Aneth Komba, alisema vitabu vitatu vilivyozinduliwa ni Riwaya, Ushairi na Hadithi za watoto na kati ya hivyo viwili vilishinda tuzo huyo 2023 na kingine mwaka huu.

"Vitabu vilivyoshinda cha riwaya ni Gereza la Kifo, Ushairi Mtale wa Ngariba, na Hadithi ni Zawadi, pia nakala 140,000 za kila kitabu zimechapwa kwa fedha za serikali ambazo ni Sh. milioni 400," alisema Dk. Aneth.



# TAKUKURU yarejesha fedha za dawa zilizoibwa

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imeokoa zaidi ya Sh. milioni 4 zilizotolewa kwa ununuzi wa dawa za Zahanati ya Orkirung'rung Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara.

Kwa mujibu wa Kaimu Mkuu wa TAKUKURU wa Mkoa wa Manyara, Bahati Haule, fedha hizo ziliibwa na kuokolewa na taasisi hiyo katika kipindi cha Julai hadi Septemba mwaka huu.

Haule, alisema fedha hizo ni kati ya Sh. milioni 13.879 zilizookolewa taasisi hiyo mkoani humo kwa kipindi hicho cha miezi mitatu.

Alisema katika kipindi hicho, taasisi hiyo ilifuatilia miradi ya maendeleo 20 yenye thamani ya Sh. bilioni 4.770 kati ya hiyo, 10 yenye thamani ya Sh. bilioni 1.928, ilibainika kuwa na mapungufu.

Katika hatua nyingine; TAKUKURU Manyara imeonya itachukua hatua kali kwa wagombea watakaotoa rushwa na wananchi watakaopokea katika kipindi cha uchaguzi wa serikali za mitaa kwa kuwa ni uhujumu uchumi.

**Katika hatua nyingine; TAKUKURU Manyara imeonya itachukua hatua kali kwa wagombea watakaotoa rushwa na wananchi watakaopokea katika kipindi cha uchaguzi wa serikali**

Haule alisema kulingana na ibara ya 4 ya Katiba ya nchi, Tanzania ni nchi ya kidemokrasia.

Ibara ya 9, inasema jukumu kubwa la serikali ni kuondoa rushwa nchini, ibara ya 8, serikali itapata madaraka kwa wananchi na itawajibika kwa wananchi.

Alisisitiza kuwa TAKUKURU imejipanga kimkakati kudhibiti rushwa kabla, wakati na baada ya uchaguzi.

"Hatua stahiki zitachukuliwa dhidi ya wagombea na wananchi watakaojihusisha na rushwa," alisema Haule.

Aliwataka wananchi wasikubali kudhalilisha utu wao kwa kupewa pombe, kanga, vyakula na vitenge ili wampigie kura mgombea maana watu wa namna hiyo ni donda ndugu lisilokuwa na tiba.



Rais wa Klabu ya Lions ya Moshi-Kibo, Julian Jones (kushoto), akikabidhi tiketi ya ndege kwa Dovotha Chuwa (katikati), mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro juzi, kabla ya kuanza safari yake kwenda nchini India, kwa ajili ya matibabu ya moyo, zilizotolewa na klabu hiyo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo familia ya Chuwa. Kulia ni Katibu wa Klabu hiyo, Yunas Swai. **PICHA: JAMES LANKA**

# Wataalamu ununuzi, ugani wanolewa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KATIBU Tawala Mkoa wa Arusha, Missaile Mussa amewataka wataalamu wa ununuzi na ugavi kuepuka kuzalisha hoja za ukaguzi na halmashauri kupata hati chafu kwenye miradi.

Mussa alitoa wito huo jana jijini hapa wakati wa kufunga mafunzo ya wataalamu wa ununuzi na ugavi mkoani hapa.

Mafunzo hayo yalihusisha pia wataalamu wa Mfumo wa Kieletroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST).

Alisema kufanya kazi kwa weledi, maadili na kuzingatia misingi ya taaluma za ununuzi, kutasaidia kuokoa fedha za serikali zinazotolewa kutekeleza miradi ya maendeleo nchini kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

"Ni aibu kwa maofisa ununuzi kusikia hamjasajiliwa na Bodi ya PSPTB (Bodi ya Ununuzi) hasa kwa Mkoa Arusha, hakikisheni mnajisajili ili tupunguze hoja za ukaguzi, lakini kuweni makini katika mikataba kwenye miradi inayoletwa huku kwenye halmashauri," alisema

Alisisitiza matumizi ya NeST kwa kuwa sio kichaka cha wizi bali unasaidia kudhibiti wizi kwa watendaji wasiokuwa waaminifu. "Weledi na maadili ni msingi mkubwa katika kuhakikisha miradi inatekelezwa ikiwa na viwango bora, hivyo lazima eneo la manunuzi liangaliwe vizuri na ikibainika kuna ukiukwaji wa sheria, wahusika watachukuliwa hatua za kinidhamu," alisema

Mkurugenzi Mtendaji wa PSPTB, Godfred Mbanyi, alisema bodi hiyo katika ukaguzi wake hivi karibuni, ilibaini baadhi ya maofisa manunuzi na ugavi hawasajiliwa.

Mbanyi alitumia fursa hiyo kuwa maofisa hao kila mmoja kuhahikisha anafuata sheria kwa kujisajili ili kuepuka kukumbana na adhabu.

Alisisitiza maofisa hao kuheshimu kanuni na taaluma zao ili sekta ya manunuzi inakuwa muhimu kufanya kaguzi kwa usahihi na kupunguza hoja za ukaguzi.

"NeST ni muhimu katika sekta ya manunuzi, lakini pia tunasisitiza wataalam kuzingatia mkataba na kupunguza hoja," alisema.

# Vijiji vyapewa mbinu za kutokomeza udumavu

**Na Allan Isaack,** SIMANJIRO

WAKULIMA na wafugaji zaidi ya 8,000 wa vijiji 10 wilayani hapa Mkoa wa Manyara wamepatiwa mafunzo ya mbinu za kilimo ikolojia, usimamizi bora wa malisho kwa mifugo na lishe ya mama na mtoto.

Mafunzo hayo yametolewa na Shirika la Kilimo Endelevu Tanzania (SAT), kwa ufadhili wa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP).

Mwezeshaji wa mafunzo kutoka SAT, Yohana Malechela, akizungumza jana wakati akitoa mafunzo hayo katika Kijiji cha Kiruani Kata ya Msitu wa Tembo, alisema kupitia mradi wa urejeshaji wa kilimo ikolojia (MUKI), wametoa elimu kwa wakulima wa vijiji 10 vilivyopo wilayani hapa.

Malechela, alisema wametoa mafunzo kwa wakulima hao 8,618, kati ya hao wanaume 3,663 na wanawake 4,965.

Alitaja vijiji vinavyotekeleza MUKI kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia 2024/2025 kuwa ni Kiruani, Ruvuremiti, Kandasikira, Kambi ya chokaa, Naberera, Lemkuna, Narakauwo na Nadonjoke.

Alisema lengo la mradi huo ni kuwajengea uwezo wakulima na wafugaji wa mbinu endelevu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi (mbinu za kilimo ikolojia), matumizi ya teknolojia za uhifadhi wa maji na udongo na kufanya urejesho wa rasilimali zilizoathiriwa na mabadiliko ya tabianchi.

“Kupitia mradi wa MUKI ili kuweza kuwafikia wakulima na wafugaji 10,000 tulitoa mafunzo kwa wakulima wawezeshaji (wakulima viongozi) ambao tunawatumia kama wawezeshaji jamii 300 katika vijiji vya mradi na kila kijiji tulichagua wakulima na wafugaji 30 walojifunza na kwenda kutoa elimu kwa wenzao,” alisema.


Ofisa Lishe Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Eshimuni Swai, alisema kama shughuli za kilimo zisipofanyika vizuri hasa utumiaji dawa kuna uwezekano wa walaji wa chakula kupata madhara makubwa kutoka na kemikali zinazotumika kuzalisha mazao.

“Tukitumia kilimo ikolojia naona kitasaidia kuboresha masuala ya lishe kwa kuwa itasaidia kuepusha wananchi kutumia vyakula vyenye kemikali nyingi,” alisema Swai.

Alisema kilimo hicho, kitawasaidia wananchi kuboresha upatikanaji wa chakula kwa kuwa kitapatikana kwa wingi na salama kwa matumizi ya binadamu.

“Kupitia kilimo hiki wananchi watapata vyakula mchanganyiko, kuboresha afya ya mama na mtoto hivyo kupunguza udumavu kwa watoto kupatiwa chakula cha aina moja kila mara,” alisema.

Clementina Kolila, Ofisa Kilimo wa Kijiji cha Kiruani, alisema elimu iliyotolewa imeleta matokeo chanya kijijini hapo kwa wafugaji na wakulima kuanza kutumia mbinu za kilimo ikolojia na lishe.





Fundi akijenga jengo la choo cha zahanati mpya ya Kijiji cha Nyasaungu, Wilaya ya Musoma mkoani Mara mapema wiki hii, ambayo iko katika hatua za mwisho za ujenzi wake. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafungwa kwa kubaka watoto

**Na Waandishi Wetu,** MWANZA

SAMWEL Anthony (34), Mkazi wa Kijiji cha Shilima Wilaya ya Kwimba mkoani hapa, amehukumiwa kifungo cha maisha jela baada ya kukutwa na hatia ya kumbaka mtoto mwenye umri wa miaka minane.

Hukumu hiyo imetolewa katika Mahakama ya Wilaya ya Kwimba na Hakimu Mkazi Mkuu, Ndeko Dastan baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili na kujiridhisha pasipo kuacha shaka kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo.

Awali akisoma mashtaka dhidi ya mshtakiwa huyo, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Juma Kiparo alidai kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo Agosti 16, mwaka huu katika Kijiji cha Shilima.

Kiparo alidai kuwa mtoto huyo alibakwa na mshtakiwa huyo baada ya kutumwa na mama yake dukani.

Alidai kuwa wakati anarudi nyumbani, mshtakiwa huyo alimvuta nyuma ya nyumba ya baba yake, kisha kumbaka.

Kiparo, alidai mshtakiwa huyo alifikishwa mahakamani hapo Agosti 23, mwaka huu na kusomewa shtaka hilo.

Hakimu Ndeko baada ya kusikiliza mashahidi watano wa upande wa Jamhuri, akiwemo mwathirika wa tukio hilo na mshtakiwa alijiridhisha pasi na kuacha shaka kuwa alitenda kosa hilo.

Kabla ya hukumu hiyo kutolewa, mshtakiwa huyo aliiomba mahakama impunguzie adhabu kwa madai kuwa ni mgonjwa na ana watoto watano akiwamo mlemavu na mdogo wake mgonjwa, wanamtegemea.

Hakimu Ndeko, alitupilia mbali utetezi huo na kumhukumu mshtakiwa huyo kifungo hicho jela na kuwa fundisho kwake na watu wengine wenye tabia kama yake.

**Mutafungwa alisema baada ya bibi huyo kufika nyumbani mtuhumiwa huyo ambaye ni jirani yake, alimkuta akinywa pombe na kumkaribisha na kupata pamoja kilevi hicho.**

Wakati huo huo; Mahakama hiyo, imemuhukumu kifungo cha miaka 30 jela, Mkazi wa Sumve, Kulwa Nkingwa (30) maarufu Maduka kwa kumbaka mtoto wa kike wa miaka 11 nyumbani kwa mganga wa jadi.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo Mei 6, mwaka huu nyumbani kwa mganga huyo (sangoma), Aloyce John katika Kijiji cha Sumve ambako mtoto huyo alikuwa amepelekwa kutibiwa.

Mshtakiwa huyo alifikishwa katika mahakama hiyo, Julai 2 mwaka huu na kusomewa shtaka la kubaka na Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Juma Kiparo mbele ya Hakimu Dastan.

Kiparo alidai kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo kinyume na kifungu cha 130.

Aliiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo kwa kuwa kosa hilo linahusisha ukatili wa kijinsia na kuwa binti huyo ni mdogo na kitendo hicho kimemuathiri kisaikolojia. Kabla ya hukumu hiyo ya kesi ya jinai namba 12898/2024, kutolewa Hakimu Ndeko, alimpatia fursa mshtakiwa huyo kujitetea ili apunguziwa adhabu.

Katika utetezi wake, mshtakiwa huyo aliiomba mahakama hiyo impunguzie adhabu kwa madai kuwa ni kosa lake la kwanza na ana famuilia inayomtegemea.

Hakimu huyo alitupilia mbali utetezi huo kwa kile kilichoelezwa kuwa ni kukosa mashiko, hivyo kumuhukumu mshtakiwa huyo kutumikia kifungo hicho jela ili iwe fundisho kwake na kwa watu wengine wenye tabia kama yake.

**Imeandikwa na Vitus Audax na Neema Emmanuel, Mwanza.**

# Gereza ladaiwa mamilioni ya maji

**Na Rose Jacob,** MWANZA

GEREZA la Butimba mkoani hapa litaanza kuondokana na adha ya maji na kudaiwa mamilioni ya fedha baada ya kujengewa kisima cha maji safi kwa ajili ya matumizi ya wafanyakazi wake na wafungwa.

Akizungumza wakati wa kukabidhiwa kisima hicho kilichofadhiliwa na Taasisi ya The Desk and Chair Foundation na vifaa vya kuanzisha elimu ya watu wazima katika gereza hilo, Mkuu wa Magereza Mkoa wa Mwanza, Masoud Kimalo, alisema kuwa wameanza kuondokana na adha ya deni la zaidi ya Sh. milioni 400 wanalodaiwa na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mjini Mwanza (MWAUWASA)

Kimalo, alisema usafi wa mazingira katika vyoo vya ndani ya gereza hilo utaimarika kufuatia miundombinu inayohitaji maji kwa asilimia 100.

Alisema wafungwa kwa sasa watakuwa na uhakika wa kufua nguo na kuoga kwa kutumia maji hayo na kuondokana na magonjwa ya milipuko na ya ngozi.

Mwenyekiti wa Taasisi hiyo, Sibtain Meghjee, alisema ujenzi wa kisima hicho ulianza Mei 6, mwaka huu na kukamilika kwake kutanufaisha zaidi ya watu 3,000 kwa kuteka maji kwa siku.

Meghjee, alisema ujenzi huo umegharimu Sh. milioni 40 kwa kuweka tangi lenye ujazo wa lita 10,000, kuunganisha maji kwenye ofisi za Magereza na malipo ya umeme wa Luku Sh. 550,000, ujenzi wa tangi jipya lenye ujazo wa lita 15,000.

# Serikali yasisitiza ushirikino na wanahabari

**Na Grace Mwakalinga**

SERIKALI imesisitiza kuwa dhamira yake ni kushirikiana na vyombo vya habari ili waandishi wafanye kazi kwa weledi, uhuru na kuzingatia sheria kwa lengo la kukuza uzalendo na kulinda taswira ya nchi.

Waziri wa Habari, Mawasiliano, na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa, alitoa msisitizo huo jana jijini Dar es Salaam, wakati wa kikao na wajumbe wa Muungano wa Haki ya Kupata Habari (CoRI), unaojumuisha mashirika yakiwamo, Baraza la Habari Tanzania (MCT), Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), Jamii Forums, Sikika, na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC).

Waziri Silaa alisema wizara hiyo inatekeleza maono ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha waandishi wa habari na vyombo vyao vinafanyakazi kwa uhuru.

"Sote tutakumbuka Rais Dk. Samia wakati anaingia madarakani, alifungua vyombo vya habari vilivyofungiwa kutokana na sababu mbalimbali na alifanya hivyo akitambua mchango wenu katika kuhabarisha wananchi na kutoa ajira," alisema Silaa.

Aliongeza kuwa wizara inatambua nia ya Rais kutoa uhuru kwa waandishi ni kuwapa Watanzania haki ya kupata habari bila vikwazo.

Mwenyekiti wa CoRI, Ernest Sungura, ambaye pia ni Katibu Mtendaji wa MCT, alisema kikao hicho kilikuwa fursa ya kuimarisha ushirikiano baina ya wizara na wadau wa habari.

"Tangu uteuzi wake, wadau tulitambua umuhimu wa kushirikiana naye ili kuimarisha ushirikiano huu, ameridhia na katika maelezo yake, ameonyesha dhamira ya kufanya kazi nasi, leo (jana), ni nafasi ya kujadili changamoto na mafanikio katika kuendeleza sekta yetu," alisema Sungura.

Akizungumzia mipango ya baadaye, Sungura alisema: "Tunapanga kuwa na vikao kazi vya mara kwa mara na Waziri Silaa ili kuimarisha zaidi uhusiano wetu utakaotuwezesha kutimiza majukumu yetu ya kuhabarisha wananchi ipasavyo".

Katika kikao cha wadau kilichofanyika wiki hii jijini Dar es Salaam, Waziri Silaa alisisitiza ahadi ya serikali ya kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari, akieleza mabadiliko yaliyofanywa yanalenga kulinda haki za waandishi wa habari na kukuza uhuru wa vyombo vya habari.

Alisema mageuzi ya hivi karibuni katika sekta ya habari yanalenga kuhakikisha waandishi wa habari wanakuwa na uhuru wa kujieleza, kupata habari, uhuru wa uhariri bila hofu ya kufunguliwa mashtaka.

Mfumo wa vyama vingi vya siasa usitupasue




Ukurasa 13

BUFE
IJUMAA NOVEMBA 22, 2024
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 12

**Pata simulizi ya Rais Samia, mabonde na milima hadi kuyaona maendeleo**

MKIMBIZI MTOTO HADI JAJI RAIA...

# Kamhadaa baba aliyeukataa uanasheria, akampa ukweli miaka 30 yuko maarufu

- Siku ya simulizi mzazi hoi kwa kicheko
- Wa kwanza kumiliki kampuni uwakili kwao
- Kapitia ubalozi, mtaalam wa wakimbizi

**Na Christina Mwakangale**

JAJI Tujilane Chizumila, ana simulizi tangu akiwa na umri wa miaka 12 akiwa mkimbizi. Ameishi Tanzania wakiwa ni wakimbizi pamoja na wazazi wake, kutoka nchini Malawi.

Leo hii ana umri miaka 71), anaisimulia Nipashe, jijini Dar es Salaam, kuhusu safari yake kutumishi masuala mbalimbali kama vile, jinsia, diplomasia na sheria. Ana uwezo wa kuzungumza lugha takribani nne; Kiingereza, Kiswahili, Kijerumani na Kichewa, na kukielewa vyema kiyao.

Mazungumzo maalum ya mwandishi wa makala hii na Jaji Chizumila, wiki jijini, Dar es Salaam yalikuwa hivi:

**Swali: Umetunga kitabu chako kichwa cha habari kinasema 'From A Refugee Girl to A Judge: My Journey' una maana gani kwa lugha rahisi?**

**Jibu:** Nimemaanisha kwamba mimi nilikuwa mkimbizi mtoto 'a child refugee' kuanzia miaka 12. Hapa Tanzania nilikuja na wazazi wangu, baba yangu alikuwa ni Mkuu wa Itifaki wa Kwanza wa Malawi, baada ya kuwa mwalimu ndipo akachaguliwa kwenda Umoja wa Mataifa (UN), New York, Marekani, kuwakilisha nchi yetu.



Jaji Tujilane Chizumila. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

Lakini baada ya mwaka, kukatokea vurugu kati ya rais Dk. Banda (Kamuzu) na mawaziri wa wakati huo, kwa hiyo ikaathiri wote ambao walikuwa ndio marafiki zao waliosoma pamoja.

Baba yangu akaitwa arudi, lakini alipigiwa simu na wenziwe kwamba asirudi, kwa sababu serikali ilikuwa imekwishandaa magari mawili, moja kutubeba na mama yangu na sisi kutupeleka kijijini na lingine kumpeleka baba kwenda kumfunga.

Kwa hiyo, akimbie! Baba akatuambia tunatoroka tunakuja Tanzania kuwa wakimbizi. Najivunia kwa serikali ya Tanzania na UNHCR, kwa kutupokea na mpaka leo nimekuwa Jaji ambaye kwa sasa ni miongoni mwa majaji wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (makao yake makuu jijini Arusha).

**Swali: Uliwahi kuwa raia wa Tanzania, sasa ni raia wa Malawi, Je, imekuwaje?**

**Jibu:** Niliwahi kuwa raia wa Tanzania, kwa sababu niliolewa na Mtanzania (tena Msukuma... (akionyesha kicheko kidogo). Niliolewa mwaka 1975 nina watoto wawili, baada ya miaka kadhaa tulitengana na nikaamua kurudi nyumbani na kurudisha uraia na kurudi Malawi.

**Swali: Tukirudi katika 'status' yako kwenye 'cv' (wasifu) wako ulikuwa jaji na sifa zingine unazungumziaje, haki za binadamu mambo kisheria? Uliipenda hii kazi?**

**Jibu:** Wakati baba kuwa amekwenda UN sisi (watoto) tulibaki na mama (Malawi), tukamfuata baada ya miezi kadhaa tukafika New York. Mimi nilikulia sana kijijini kwa mama yangu.

Kwa sababu miaka ya 1950 wakati mimi na wadogo zangu wanazaliwa, mimi nilikuwa wa kwanza na baba alikuwa anasoma Chuo Kikuu cha 'Salisbury' ambacho sasa ni Harare huko Zimbabwe,na baadaye akaendelea kwenda kusoma Lesotho na kisha Afrika Kusini.

Wakati huo ukumbuke tulikuwa chini ya 'Federation', Umoja wa Nyasaland, ambayo ni Malawi sasa hivi, Northern Rhodesia ambayo ni Zambia sasa na Southern Rhodesia ambayo ni Zimbabwe. Tulikuwa hatuna chuo kikuu, kwa hiyo ilibidi kupita huko.

Wakati baba anasoma alitupeleka nyumbani kwa mama yangu kwa babu na bibi mzaa mama. Babu alikuwa ni mwalimu wa shule ya msingi na mama. Nilikaa sana kijijini, baadae aliporudi kutoka masomoni tukahamia Zomba, ambao ulikuwa mji mkuu wa Malawi wakati huo, kabla ya kuhamishiwa Lilongwe.

Kwa hiyo, kuwa mtoto wa kukulia kijijini tumefika New York, unafungua macho unaiona, tulisoma tu kwenye jiografia,

INAENDELEA UK.14

UCHUMI

MUUNGANO ULIKOANZA HADI ULIKOFIKA...

# Pata simulizi ya Rais Samia, mabonde na milima hadi kuyaona maendeleo

**Na Mwandishi Wetu**

TANGANYIKA na Zanzibar zilipoungana na kuunda Jamhuri ya Muugano Tanzania, Rais Dk. Samia Suluhu Hasan, ana ufafanuzi wake kuhusu mitaji yake ya maendeleo, akiitaja kadhaa; ushirikiano wa kihstoria, umoja wa pande hizo mbili na kundi la vijana.

"Fikra zangu hutawaliwa na picha ya vijana wanne kutoka pande zote mbili za Muungano. Vijana hao, wawili wa kiume na wawili wa kike, waliomsaidia Mwalimu Julius Nyerere kuchanganya udongo wa Tanganyika na Zanzibar, kutoka kwenye vibuyu viwili ..." anatamka.

"Baada ya kuuchanganya, hakuna teknolojia inayoweza kuurudisha udongo ule," anaongezea, katika hotuba ya Muungano, Aprili mwaka huu, akiusifu:

"Ni 'Muungano maalumu na wa kipekee' katika misingi ya utu, udugu, na umajumui wa Afrika (Pan-Africanism), umeweza kushinda majaribu mengi ya kuuvunja," anatamka.

Rais Dk. samia anakumbusha wakati wa Muungano, Tanganyika na Zanzibar zilikuwa katika viwango duni vya maendeleo, wananchi wengi walikuwa masikini, akiongeza:

"Sekta za uzalishaji hususan kilimo kilikuwa chenye tija ndogo na hapakuwa na miundombinu ya kutosha ya usafiri na usafirishaji. Huduma za kijamii, elimu, afya, maji na umeme pia zilikuwa adimu na za kibaguzi."

Anataja jukumu la kwanza baada ya Muungano lilikuwa kujenga uchumi endelevu na unaowanufaisha wananchi wote bila ya ubaguzi, wakiimarisha na kupanua huduma za kiuchumi na kijamii, kuwaongezea kipato wananchi.

"Jitihada zilizofanywa ndani ya miaka hii 60 zimesaidia kukuza Pato la Taifa kufikia Shilingi Trilioni 170.3 kwa takwimu za mwaka 2022, na pato la mtu mmoja mmoja kufikia wastani wa shilingi milioni 2.8 kwa mwaka 2022.

### YALIYOIBUA MAENDELEO

Hapo Rais Dk. Samia, mzaliwa wa Zanzibar, anataja eneo mojwapo lilioibua maendeleo ni imani na dhamira ya waasisi na viongozi wake, Mwalimu Julius Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume.

"Walikuwa mstari wa mbele katika kudai uhuru kupitia vuguvugu la Umajumui la Afrika Mashariki na Kati, yaani Pan African Movement of Eastern and Central Africa, au kwa ufupi PAFMECA.

"Lengo la PAFMECA lilikuwa kujenga umoja, mshikamano na ushirikiano miongoni mwa watu wa Afrika waliokuwa chini ya utawala wa kikoloni wakidhamiria kuunganisha nchi zao mara baada ya kupata uhuru," anasema.

Pia, anatafsiri suala la undugu wa kihistoria, Tanganyika na Zanzibar, waliotenganishwa na mipaka ya ukoloni, lakini kwa asili walikuwa jamii moja.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika tukio la kuadhimisha miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, mwaka huu jijini Dar es Salaam. **PICHA:MTANDAO**

> **"Aidha, magonjwa kama vile UKIMWI, Kipindupindu, Homa ya mafua ya ndege, na hivi karibuni Uviko 19, nayo yalitikisa Taifa letu.**

### KINACHOENDELEA SASA

Rais Dk. Samia anataja kuwapo Tume ya Pamoja chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, inayosikiliza na kutatua changamoto za Muungano zinapojitokeza.

Hapo anataja kuanzia mwaka 2021 hadi Aprili mwaka huu, kuwapo hoja 15 kati ya 18 zimeshapatiwa ufumbuzi. Tume iliyoundwa inafanya kazi ya kulinda dhamira ya udumishaji muungano nchini.

Eneo lingine Rais Dk. Samia analitaja katika Muungano, ni kuiwezesha Tanzania kuwa na ushawishi mkubwa kikanda na kimataifa, akinena kupitia nguzo ya Diplomasia ya Uchumi, imevuta mitaji, uwekezaji, teknolojia, soko la bidhaa na huduma zitokazo nchini.

Hapo ndipo anataja zao mojawapo ni Tanzania kuufikia Uchumi wa Kati, tangu zama Serikali Awamu ya Tano, Dk. Samia akiwa Makamu Rais.

Hapo ana ufafanuzi, kupitia hotuba yake : "Nafarijika kwamba kwa sasa nchi yetu imefikia Uchumi wa Kati katika ngazi ya chini na jitihada zetu zote sasa kufikia uchumi wa kati, ngazi ya juu.

"Wastani wa umri wa kuishi (life expectancy) wa Mtanzania umeongezeka kutoka wastani wa miaka 45 mwaka 1964 hadi wastani wa miaka 67 mwaka 2024.

"Sensa ni moja kati ya mambo ya Muungano. Hadi sasa, zimefanyika sensa za watu na makazi mara sita. Sensa ya kwanza ilionyesha Tanzania kuwa na watu milioni 9.6 na ile ya mwisho 2022 imetuonyesha idadi ya Watanzania kuwa milioni 61.741," anaeleza.

Anaitaja kuwa ni taarifa yenye msaada mkubwa kwa mipango ya kiserikali na kutuongoza matumizi ya rasilimali:

Pia, anataja serikali mbili nchini, zimeendelea kuibua na kutekeleza programu na miradi inayolenga kupunguza umaskini wa kipato, inainua ubora wa maisha na ustawi wajamii kwa pande zote mbili za muungano.

Kwa upekee, anaugusa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), uliotekelezwa kwa awamu tatu sasa, umeonyesha uwezo wa kaya kumudu gharama za mahitaji ya msingi umeongezeka.

"Vilevile matumizi ya pembejeo yameongezeka, hivyo kuongeza tija kwenye kilimo, na matumizi ya huduma za afya pia yameongezeka na mahudhurio shuleni kwa watoto nao umeongezeka," anasema.

Kwa mujibu wa Rais Dk. Samia, miradi mingine iliyotekelezwa katika pande zote mbili, inajumuisha Programu ya Usimamizi wa Bahari na Pwani (MACEMP) na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo na Sekta ya Mifugo (ASDP - L).

Vilevile, anaitaja Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani ya Mazao na uboreshaji wa Huduma za Fedha Vijijini (MIVARF); Mradi wa Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Zao la Mpunga (ERPP); na Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Maeneo ya Pwani (LDCF).

Ni orodha ndefu inayojumuisha, Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDCF), mfumo wa Wabunge, unaowanufaisha wananchi katika sekta za afya, maji, ajira, elimu na miundombinu.

Katika elimu ya juu, Rais Dk. Samia akataja kuwapo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pekee wakati nchi zinaungana mwaka 1964, lakini kutimu miaka 60 ya Muungano kuna vyuo vikuu 49, vikiwamo 19 vya umma na 30 binafsi. Kati yake, 46 viko Tanzania Bara na vitatu Zanzibar."

"Mwaka 2023/24, kulikuwa na jumla ya wanafunzi wa elimu ya juu 240,523, ikilinganishwa na wanafunzi 14 tu waliokuwapo wakati nchi zetu zinaungana" anatamka Rais Dk. Samia.

"Tangu kuanzishwa Bodi ya Mikopo mwaka 2004, wanafunzi wapatao 705,622 wamepatiwa mikopo yenye thamani ya shilingi trilioni 6.69, wanufaika wanawezeshwa kusoma kwenye vyuo vya Serikali na binafsi," anasema Rais Dk. Samia.

### JINSIA NA UTUMISHI

Katika eneo hilo, akiweka rekodi kuwa rais wa kwanza nchini mwanamama, anasema: "Suala la usawa wa kijinsia zote liliingizwa kwenye Katiba, hatua iliyowezesha uwakilishi wa wanawake bungeni kuongezeka."

Anafafanua ni kutoka watatu mwaka 1964 kwenye bunge la kwanza la Muungano, hadi wanawake 148 (asilimia 37.75) ya wabunge wote 392.

Rais Dk. Samia anaendelea: "Wakati huo, hapakuwa na mwanamke yeyote kwenye uongozi wa mihimili ya dola, yaani Serikali, Bunge na Mahakama.

"Leo hii, kati ya mihimili mitatu ya dola, wanawake wanaongoza mihimili miwili, Serikali na Bunge, jambo linalothibitisha kuendelea kuimarika kwa usawa wa kijinsia," anafafanua

### MAPINDUZI YA MAWASILIANO

Rais Dk. Samia anaeleza kushamiri miliki ya simu za mkononi kwa umma, wamiliki wakiongezeka, ikikadiriwa kuwapo laini za simu zaidi ya milioni 72 na watoa huduma wameongezeka hadi watano, wakiwa na huduma zenye kasi mpya inayoitwa 5G.

"Kiasi cha laini milioni 53 zimesajiliwa kutumia huduma za kifedha kupitia simu za mkononi," anaongeza Rais, akiitolea ufafanuzi, ngazi ambayo sasa asimilia 98 ya Watanzania vijijini wananufaika.

"Maendeleo haya yamechangiwa na uamuzi wa serikali kuanzisha Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, maarufu UCSAF wenye jukumu la kuimarisha miundombinu ya mawasiliano vijijini.

"Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2009 UCSAF imeweza kujenga minara 1,435 iliyowezesha zaidi ya wananchi milioni 16 katika kata 1,306 na vijiji 3,838 kupata mawasiliano ya uhakika.... na sekta binafsi zimewezesha kuimarika kwa huduma."

### CHANGAMOTO ZAKE

Rais anataja katika miaka 1970 hadi 1980, Muungano nchini ulikumbwa na changamoto kama; ukame na njaa (hasa 1974 ), mtikisiko na anguko la uchumi duniani, bei ya mafuta na vyakula kupanda duniani, ukiumiza uchumi nchini.

Lingine linaloambatana nayo, mwaka 1977 Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ilivunjika, hata kuilazimu serikali kugharamia upatikanaji huduma za EAC, huku mwaka mmoja baadaye, ikazuka vita dhidi ya utawala wa Idd Amin wa Uganda.

Hapo Rais anaitolea ufafanuzi: "Fedha zilizotengwa kwa maendeleo yetu na rasilimali nyingine zikaelekezwa kugharamia vita hivyo.

"Vilevile, kwa nyakati mbalimbali, katika soko la dunia tulikumbana na anguko kubwa la bei za mazao yetu ya biashara kama vile chai, mkonge, kahawa, karafuu na pamba, hali iliyoathiri ukuaji uchumi wetu uliokuwa unaimarika vizuri.

"Aidha, magonjwa kama vile UKIMWI, Kipindupindu, Homa ya mafua ya ndege, na hivi karibuni Uviko 19, nayo yalitikisa Taifa letu.

Kwa upande mwingine, miaka ya 2001 hadi 2007 tulipata changamoto ya kisiasa Zanzibar, iliyosababisha baadhi ya washirika wetu wa maendeleo kusitisha misaada.

Mambo haya yote, yalitufanya tuunge nguvu kitaifa, tuimarishe umoja na mshikamano wetu, uliotujengea uwezo wa kuhimili kadhia zote hizo, na kulivusha Taifa letu likiwa salama na imara zaidi."

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Mfumo wa vyama vingi vya siasa usitupasue






NA JOSEPH KULANGWA
(+255) 713 410008
kulangwasos@gmail.com

HIVI karibuni, Waziri mwenye dhamana ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, alinikumbusha jambo zuri sana katika historia ya nchi.

Mchengerwa alisema kiini cha kuwa na ofisi hiyo, ni kutokana na wazo la Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere la kupeleka madaraka kwa wananchi wa chini, yaani waishio mitaani.

Alikuwa akizungumzia mbilingembilinge iliyoko mitaani sasa hususan katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu mwakani.

Akasema Mzee Nyerere, alitaka kuona watu waishio pamoja vijijini, mitaani na vitongojini, wakijichagulia viongozi wao waliowaamini hasa kutokana na kuzoeana, pia na kuishi pamoja kwa muda mrefu.

Mchengerwa akadokeza, kuwa hali hiyo ilijiri hususan kipindi kile akiwapo Mwalimu Nyerere na watu kuchaguana bila matatizo yoyote na kupata viongozi wazuri na rahim.

Hali hiyo ilianza kipindi kile nchi ikitawaliwa na chama kimoja, enzi hizo TANU na baadaye kuzaliwa CCM baada ya muungano wa vyama vya TANU ya Tanganyika na ASP ya Zanzibar mwaka 1977.

Nayo CCM ikaongoza peke yake mpaka ilipotimu mwaka 1992 tuliporejea kwenye mfumo wa vyama vingi vya siasa, waliokuwa hawana vyeo kutokana na kutokuwa wanachama wa CCM nao wakaanza kuvipata.

Wakaibuka wenyeviti, makatibu wakuu na wengineo wakiwakilisha vyama vyao, lakini kipinzani. Na hata uchaguzi nao ukaanza kujigawa kipinzanipinzani hivi, kwamba kama wewe si mwana wa chama fulani, hufai kuongoza.

Gonjwa hilo likaendelea kututafuna mpaka sasa, hata ukifika uchaguzi, ule utanzania wetu unatoweka na kuanza kutazamana kama wenyeji na wakimbizi, ambao mpinzani anakuwa mkimbizi na mwana anachokitaja yeye anabaki kuwa mwenyeji.

Kifupi ikawa kwamba kama wewe si mfuasi au mwumini wa chama asichokitaka, basi hufai hata kulumangia, kwamba hustahili kuwa kiongozi katika nchi hii na siku zote utasimangwa na kusukwasukwa, huenda ikiwa ni pamoja na hata kupata misukosuko.

Mwaka fulani donda letu likaanza kutoka usaha na miaka iliyofuata likatumbuka kabisa na kutuanika Watanzania tulivyooza kisiasa, ukianika kasoro zizisofaa kutambulishana hata kidogo.

Ulipofika uchaguzi ikawa balaa, tunaonana kutoka kundi ligine kisiasa unabaki kuwa kuonekana mbumbumbu usiyestahili, una sifa ya ungumbaru wa kusoma, hadi kuandika, hivyo kushindwa kujaza fomu ya ugombea.

Mtu akabeba sifa hakujua alizaliwa lini na wapi na umri wake kumruhusu kugombea uongozi wa Taifa alimozaliwa, akaenguliwa na kutupwa jalalani kumpisha wa kundi jingine, anayepata urahisi kama wa kupita bila kupingwa.

Mwaka huu sana, yanameonekana tena ya waliokuwa wakishangiliwa kusoma vizuri risala, uchaguzi umefika. Ndio hilo sasa hawajui tena kusoma wala kuandika na hawafai kugombea kuongoza hata mitaa!

Kosa dogo la herufi linatosha kukuengua usigombee. Umekosea tu namba ya mwaka hufai kugombea! Utadhani sijui wanatafutwa viongozi wenye akili mnemba?

Katibu Mkuu wa CCM, Dk Emmanuel Nchimbi naye anashangaa kama mimi!

Kawaambia wahusika, akiwamo Mchengerwa, hebu dosari ndogondogo kama hizi tusizipe uzito sana kiasi cha kunyima wengine haki za kuwania uongozi katika Taifa lao, wanaenguliwa huku wananchi wakiwataka na hatimaye kuletewa wasiowataka! Hebu tuendelee kujifunza demokrasia, tutafika!

Tungekuwa na viongozi wengi kama Dk Nchimbi katika nchi hii, naamini makandokando kama haya yasingekuwa yanatuzibia njia ya maendeleo.

Najiuliza, hivi tukiamua kufuta vyama vyote vya siasa nchini ambavyo mimi naona ndivyo vinatugawa, tutakuwa tumepoteza nini?

Hivi mathalan ingekuwa mgonjwa akienda hospitali na kutakiwa kuandika jina lake kwenye kadi ingekuwaje?

Yaani kama sheria ingekuwa inamtaka mgonjwa akikosea jina asitibiwe, hivi hatuoni wengi tungeishia mochari?

Kama sivyo, kwa nini wasimamizi wasituhoji majina tukawambia wakaandika kuliko kututega ili tukosee watuengue? Mbona zamani mambo mengi tulitumia dole gumba na yakaenda?

Wengine wanakuja na oh kazi ya ujasiriamali haifai kukupa sifa ya kuwa mgombea, leo unakataa kutambua ujasiriamali wakati Dk. John Magufuli aliwapa Wamachinga vitambulisho vya Sh 20,000.

Rais Samia Suluhu Hassan, Mwenyekiti wa CCM Taifa, anawatambua bodaboda na kuwabatiza jina la 'Maofisa Usafirishaji', leo wewe nani unasema si kazi rasmi na si ujasiriamali, wanagombea nawaengua?

**Acheni hizo!**

# Kamhadaa baba aliyeukataa uanasheria, akampa ukweli miaka 30 yuko maarufu

INATOKA UK.11

kumbe mamabo? yako hivi, ila ilikuwa ni mshangao mkubwa sana baba amekuja 'airport' (uwanja wa ndege) na dereva mzungu (walipowasili New York)... tukasema hee baba una dereva mzungu!

Hivyo tukaenda ofisi kwake kupaona na jengo la UN lilinifurahisha sana kwa sababu limejengwa tofauti, kulinganisha na majengo mengineyo ambayo yako tu kwa 'square'(mraba).

Siku hizi kuna wabunifu tofauti, enzi hizo ilikuwa ujenzi mwingi ni 'square', ila lenyewe jengo la UN lilikuwa kama nusu mwezi mwonekano wake.

Nikasimama pale nashangaa, nitafanya nini na mimi nije nifanye kazi kama wewe! Akasema (baba) soma sana. Nilipofika huku (Tanzania), nikaingia darasa la sita, nikisoma Shule ya Msingi Chang'ombe (iliko DUCE, Dar es Salaam) hadi la saba alafu nikasoma sekondari ya Asumpta, enzi hizo ikiwa na jina hilo na baadae ikaja kuitwa Weruweru hadi kidato cha nne.

Baada ya kukaguliwa wakimbizi waliwachekecha, serikali iliwachukua ambao walikuwa na uwezo wa kufanya kazi, hivyo baba yangu alisema anaweza kufundisha, akapelekwa Old Moshi Sekondari, ndio maana nilisoma Asumpta Sekondari.

Nikaja Sekondari ya Jangwani (Dar es Salaam), hadi kidato cha sita na nikaingia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM 1977), kwa shahada ya kwanza, nikichukua sheria za kimataifa na diplomasia, kwa sababu mawazo yalikuwa kufanya kazi UN.

Pia, shahada ya pili nikafanya Sheria ya Kimataifa ya Umma. Nilifanya kazi miaka 10 na Shirika la Sheria la Tanzania (Tanzania Legal Corporation) na niliporudi Malawi nikapewa kazi kama wakili wa serikali.

Ila nilikaa nyumbani kwa mwaka mzima kwanza nikisubiri 'clearance' (kuhalalishwa) na serikali kwa sababu nilikuwa mtoto wa mhujumu wa serikalini (dissident).

Kwa hiyo, nikaja kupata kazi Save the Children Federation US mwaka 1989-1990. Nilifurahi kufanya kazi huku kwa sababu tulizifikia jamii za chini kabisa na lengo langu lilikuwa kuihudumia jamii. Baada ya mwaka ndiyo nikaitwa kufanya kazi kama wakili wa serikali.

Baadae nikapata kazi shirika la UNHCR, nikafurahi kwa sababu ilikuwa na mimi nawashughulikia wakimbizi kama mimi nilivyoshughulikiwa.

Nikafungua kampuni yangu la sheria, nikawa mwananke wa kwanza mwanasheria kufungua kampuni binafsi.

Halafu nikachaguliwa kuwa Balozi wa Malawi Zimbabwe na Southern Africa Development Corporation (SADC).

Baada ya miaka minne, nikachaguliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu, kisha nikapata nafasi kuwa 'Ombudsman' na kuwa mwanamke wa kwanza kushika nafasi hiyo.

**Swali: 'Ombudsman' ni nafasi gani hii kisheria kwa lugha rahisi?**

**Jibu:** 'Ombudsman' ni mtu anayesimamia sheria ni mtu anayeshughulikia kesi za watumishi wa umma, ambao wana madai tofauti kama mishahara au waliostaafu hawajalipwa, ambao wanapata uhamisho kwa sababu tofauti au hakuna maelewano, kati ya mtumishi na bosi.

Unakuwa unasikiliza kesi, inakuwa kama mahakama na unaweza hata kumuita rais akaja mbele yako kuja kujieleza, hata mawaziri na wenye vyeo vikubwa. Kwa Tanzania nafasi hii iko ndani ya Tume ya Haki za Binadamu imekuwa kama idara.

Baada ya hiyo kazi niliyoifanya Malawi kwa miaka mitano nikastaafu, ila nikaona kama bado nina nguvu.

**Swali: Je, ulipenda kusomea hiki unachokifanyia kazi hivi sasa?**

**Jibu:** Kusema ukweli ilikuwa ni bahati mbaya sikupenda kusoma sheria na haikuwa kwenye wazo langu. Mimi baba amenilipia ada toka tulipofika Tanzania hadi chuo kikuu, kabla ya kupata 'scholarship' ila enzi zile wazee hawakuwa wanampa nafasi mtoto kujichagulia taaluma.

Wakati najaza fomu ukiwa kidato cha sita unakuwa na machaguo matatu; chuo kikuu; ualimu na nyingine. Na hata chuo kikuu pia unachagua usome nini, baba yangu alikuwa ni profesa wa ualimu na historia pale chuo kikuu.

Alitaka niwe mwalimu. Ila mimi sikupenda, baba mwalimu, mama mwalimu, babu mwalimu, mashangazi walimu! Nikasema mimi sitaki, nilikuwa napenda jiografia nikataka niwe na kazi katika uwanja wa ndege na kufuatilia ndege zinapotua na kabla ya kupaa.

Nikaomba nifanye kazi pale pale chuo kikuu, baada ya kumaliza kidato cha sita kwa sababu sikwenda 'National Service'(JKT). Kuna siku wakati tukiwa ofisi tunachambua fomu zilizojazwa nikamwambia bosi wangu, mimi sikupenda kusoma fani hii lakini baba kanichagulia 'education' (ualimu) ila sikupenda.

Na kila nikiweka katika mfumo inakuja chaguo la kwanza, nikamwambia nifanyaje, akasema jaza fomu tutaipitia fomu. Baadaye majibu kutoka nikachaguliwa kwenda sheria, hii ilitokana na mabadiliko niliyofanya awamu ya pili.

Nikawauliza rafiki zangu jamani katika sheria si hakuna hesabu wakasema ndio, kumbe walinidanganya, unapoanza tu kusoma unakutana na mambo mengi kama 'bank statement' usipoyajua utamteteaje mteja, kwa kweli nilikatishwa tamaa ila sikuacha kuendelea kusoma sheria.

Niliporudi nyumbani, baba akabaki anashangaa mbona wewe umechaguliwa chaguo la pili badala la kwanza? Nikamwambia sijui, kumbe nilibadilisha. Baadae imepita miaka 30 nikamwita nilivyokuwa Balozi Zimbabwe, nikaja kumwambia nilibadilisha sikutaka kuwa mwalimu, alicheka sana. Hii ndio hatua niliyopita hadi kuwa mwanasheria sasa.

**Swali: Unaandika vitabu kuhusu maisha, una kitabu pia cha 'A widow's perspective - a personal experince' kwa nini?**

**Jibu:** Nilitumia hiyo 'personal experience' yangu kuwaelimisha wabunge ili wapitishe sheria yaku 'stop property grabbing' ambayo ilikuwa imeshakatiliwa kupitishwa mara ya kwanza bungeni kwasababu ilikuwa na changamoto kadhaa. Niliwahi kuuliza baadhi ya wanaume ambao ni wabunge mjane ni nani? Wakasema ni mke aliyefiwa na mume wake. Nikawaambia mwanamke yeyote anaweza kuwa mjane.

Baba mmoja kainuka akasema mimi atayemuonea mjane mama yangu hatutaelewana, nikasema kumbe umenielewa. Mjane anaweza kuwa ni binti yako, mama, dada, shangazi. Baada ya muda mfupi sheria iliyowahusisha wajane ilirudishwa bungeni na ilirekebishwa bila upinzani wowote.

**Swali: Kwenye kazi hii kuna changamoto yeyote unayokumbana nayo?**

**Jibu:** Kwanza katika kazi hii ninayoifanya ni kutofahamika kwa mahakama hii, kuna wafanyakazi wachache, suala la kifedha. Na kutokuifahamu mahakama hii kunasababisha kuwapo kwa kesi chache hasa wanawake wanashindwa kuleta kesi.

**Swali: Ulikuwa Balozi kwenye nchi ngapi?**

**Jibu:** Nilikuwa Balozi wa Zimbabwe, pia wa SADC (Southern Africa Development Community), nchi zote za kusini mwa Afrika.

**Swali: Umewezaje kufika hapo ulipo sasa, ikizingatiwa kuna dhana tofauti kuhusu mwanamke na changamoto za kuzifikia ndoto zake?**

**Jibu:** Nawashukuru wazazi wangu, linapokuja suala la kusoma hakukuwa na masihara. Na mama yangu ijapokuwa alikuwa mwalimu wa shule ya msingi alikuwa ananifundisha 'English literature' na vitabu vingi vilikuwepo nyumbani hata vitabu vya sheria, nikiwa na 'home work' yangu nampa ananisahihisha ananiambia hapa hapana rudia.

Baba pia tabia yake ilikuwa lazima uhakikishe umesoma magazeti ya siku hiyo, umesikiliza taarifa ya habari. Atakaa anakunywa chai, anawaita...anza wewe nipeni 'brief' (muhtasari) hapa nchini kuna nini na kimataifa? Anauliza shuleni mmesoma nini? Na vitabu alikuwa navyo vingi na hakukuwa na sababu ushindwe kusoma.

Kulikuwa na msukumo mkubwa kuhusu kusoma, lakini pili ni tabia walijitahidi kutuambia kwamba lazima ujiheshimu na ujitegemee akili yako. Ila nakumbuka darasa letu chuo kikuu wasichana tulikuwa sita na wanaume 40. Pia, serikali zetu siku hizi zinatupa hiyo nafasi.

**Swali: Unazungumza lugha ngapi?**

**Jibu:** Kwa kuzungumza kwa uhuru zaidi nitasema ni lugha tatu kiingereza, Kichewa, Kiswahili. Mimi ni myao wa Malawi. Na jina langu Tujilane ni la kiyao, linamaanisha 'reconciliation' (maridhiano).

Kijerumani pia najua, kwa sababu nimesoma shahada ya pili kwahiyo lugha. Ukiwa huku kwenye mahakama hii lazima ujue lugha nyingine ya AU kwa hiyo kiingereza nakijua na sasa nasomea kifaransa. Kiswahili mwaka huu kimeingizwa katika AU kwa hiyo huwa tuna wakalimani ambao wanasaidia kukalimani.

**Swali: Kazi hii unaona ina changamoto katika utekelezaji wa majukumu na maisha ya kawaida.**

**Jibu:** Tulipokuwa darasani walimu walikuwa wanatuambia ukiwa mwanasheria usipande daladala, zamani tulikuwa na mabasi yanaitwa UDA, kwa sababu huwezi kujua ndugu wa yule uliyemhukumu anaweza akakuvamia.

Kujilinda na kujitenga ni lazima. Na pia unajilinda na watu wasije wakakuona upo na mtu fulani wakasema kuna mazingira ya rushwa.




Mwandishi wa Nipashe, alipozungumza na Jaji Tujilane Chizumila, hivi karibuni katika Uwanja wa Ndege, Julius Nyerere, Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



**HABARI DODOMA**

# Chuo chaagizwa kuisadia serikali kujiimarisha kiuchumi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande amekiagiza Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini (IRDP) kufanya utafiti kwenye kodi na madini ili kuisaidia serikali kujiimarisha kiuchumi.

Chande alitoa agizo hilo juzi wakati wa uzinduzi wa Baraza la 13 la Uongozi wa chuo hicho uliofanyika mkoani hapa.

Alisema Chuo hicho kina wajibu wa kufanya utafiti na kutoa mwelekeo kwa serikali ili kuongeza mapato katika maeneo mbalimbali nchini ikiwamo kuongeza thamani kwenye vitu.

"Nawaomba mjikite kufanya tafiti kwenye sehemu hizo, mkifanikisha hilo mtakuwa mmeisaidia serikali kuongeza mapato, pia mtakuwa mmewasaidia mtu mmoja mmoja kujiinua kiuchumi," alisema Chande.

Alisema imezoeleka kuuza malighafi katika madini ya dhahabu na vitu vingine ni muhimu wataalam kufanya utafiti ili kuondoa dhana ya kuuza malighafi na kusaidia kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja kwa wachimbaji madini na mapato ya serikali.

> **"Ulaya reli ni ya serikali, mabehewa ni ubia, hivyo tuipe nafasi sekta binafsi ishiriki katika reli ibebe mizigo. Pia nashauri vipande vilivyobaki vya kujenga serikali isibebe..."**

"Inaumiza sana kuona jambo la kuuza malighafi linazoeleka,hebu watafiti fanyeni kazi ili kuisaidia serikali kuongeza mapato yake," alisema.

Aliwataka pia kuanzisha masomo kwa njia ya mtandao na matawi ya chuo nchi mbalimbali ili kusaidia kwenye elimu na utafiti.

Kwa upande mwingine, Dk. Chande, alilitaka baraza hilo kufanya kazi kwa kuzingatia sheria na miongozo inayotolewa na serikali.

Aliwashauri kutumia muda mwingi kusoma nyaraka hizo kwa kina ili kujua majukumu yao na mipaka ya utendaji ili kurahisha utendaji wao wa kazi. Alisema moja ya majukumu waliyonayo ni kuishauri menejimenti ya chuo hicho ikiwamo kujadili mambo kuhusu baraza hilo ili kutatua changamoto zilizopo.

Mkuu wa Chuo, Profesa Hozen Mayaya, alitaja baadhi ya mafanikio waliopata kuwa ni kuboresha miundombinu na matumizi ya Teknolojia na Habari na Mawasiliano (TEHAMA) chuoni hapo.

## Wahitimu CBE kujengewa uwezo kujiajiri

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA kukabiliana na tatizo la ajira kwa vijana nchini, Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kinatarajia kuboresha mitaala ili kuwajengea uwezo wahitimu kujiajiri na kukabiliana na hali ngumu ya maisha.

Mkuu wa CBE, Profesa Edda Lwoga, alitangaza mpango huo juzi kwenye kongamano la wanataaluma lililofanyika jijini hapa, ikiwa ni maandalizi ya mahafali ya 59 na maadhimisho ya miaka 60 tangu kuanzishwa kwa chuo hicho Januari mwaka 1983.

Prof. Lwoga, alisema katika kipindi cha miaka 60 ya chuo hicho, wameendelea kuboresha mitaala ili kuendena na mahitaji ya soko la ajira na kuwajengea uwezo wahitimu wao wa kujiajiri na kuajiri wengine.

"Tunataka wahitimu wetu wakitoka hapa wawe na uwezo wa kujiajiri wenyewe badala ya kusubiri kuajiriwa, hatutaki wahitimu wetu wawe watu wa kuandika barua na kuzunguka nazo hadi zinachakaa mikononi, lazima wawe na uwezo wa kujiamini na kuthubutu," alisisitiza.

Lwoga, alisema chuo kimeanzisha mpango atamizi wa bunifu za mawazo ya biashara kwa wanafunzi ili kuwasaidia kuziendeleza na kusajili biashara zao.

Alisema tangu kuanza kwa mpango huo mwaka 2022, zaidi ya vijana 400 wamenufaika kwa mawazo yao ya biashara na bunifu mbalimbali kuendelezwa na kusajiliwa.

Mkuu huyo wa CBE, aliishukuru serikali kwa kuendelea kukiwezesha chuo hicho kuboresha miundombinu na kwamba hadi sasa katika kampasi zote wana wanafunzi zaidi ya 20,000 na program za mafunzo zaidi ya 60.

Alisema katika mwaka huu wa masomo, wanafunzi 3,396 katika kampasi ya Dar es Saalam, Dodoma, Mbeya na Mwanza watahitimu masomo yao katika kozi mbalimbali.

Mkuu wa Idara ya Uatamizi wa Mawazo ya Biashara CBE, Dk. Adrian Nduguru, alisema tangu kuanzishwa kwa mpango huo mwaka 2022, umekuwa ukitoa fursa kwa wanafunzi kubuni mawazo yao ya biashara na yale yanayokidhi vigezo kuendelezwa.

"Wanafunzi wanaleta mawazo yao ya biashara na bunifu, yanashindanishwa na yale ambayo yanakidhi vigezo chuo kinayachukua, kuyasimamia na kusajili biashara," alisema Dk.Ndunguru.

Mmoja wa wanufaika wa mpango huo, Mwamini Issa, aliiomba serikali kutumia bunifu ambazo zimekuwa zikiandaliwa na vijana wa kitanzania kutatua changamoto katika jamii.



Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa (wa pili kulia), akikabidhi risiti ya ununuzi ya vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 3.9 kwa Mkuu wa wilaya ya Chamwino, Janent Mayanja, kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kupikia la Shule ya Msingi ya Wasioona ya Buigiri, wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Takwimu ya Afrika, wilayani humo, mkoani Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## RC Dendego awafunda wanafunzi vyuo vikuu

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WANAFUNZI wa vyuo mkoani hapa wametakiwa kuwa na mtandao wa watu wenye nidhamu ili kuleta heshima katika jamii.

Rai hiyo imetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego katika kongamano la wasomi na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa lililofanyika mapema wiki hii katika Chuo cha Uhasibu Kampasi ya Singida.

Dendego, alisema wanavyuo hao wanatakiwa kutumia vizuri ujana wao kwa kesho iliyo bora kwa kuzingatia uzalendo, heshima, utii, utulivu na kuwa na mtandao huo wa watu wazuri kwa manufaa yao ya baadaye.

Aliwasisitiza kujiandaa vizuri kwa kutumia elimu wanayopata vyuoni kujiajiri na kujipatia fedha kwa nguvu zao kwani kutawaletea heshima, amani na uhuru katika maisha yao.

"Msichague kazi, tujiajiri kuongeza kipato, tuchakarike vijana kuongeza kipato kwani ubora na amani ya nchi yetu ni kutupa fursa ya kupata kipato, ujana ni fedha, nidhamu na kujiamini, muda wa kuishi vyuo ni mfupi hivyo tuutumie vizuri kuandaa maisha mazuri ya baadae," alisema.

Mkuu huyo wa mkoa aliwaasa kujiepusha na mahitaji makubwa ili kuepusha gharama zisizo na msingi kwani wazazi wao wanatumia fedha nyingi kuwasomesha na si kwenda kufanya starehe vyuoni.

"Tumieni muda mwingi kujisomea kwa bidii na kuepuka mahusiano ya mapenzi vyuoni, epukeni aibu ya kufeli mitihani, vifo kutokana na ugomvi wa wivu na magonjwa ya ngono zembe," alisema.

Awali Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa ya Singida, Amaniel Samweli, akitoa elimu ya hamasa juu ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa alisisitiza kuwa ni haki yao kushiriki kuchagua viongozi na kuwahimiza kujitokeza kwa wingi siku ya uchaguzi .

Rais wa Serikali ya Wanafunzi katika Chuo hicho, Peter J. Peter na Godfrey Mtilabu, Katibu Mkuu wa Shirikisho la Vyuo Vikuu nchini (TAHLISO), waliahidi kushirikiana na serikali katika uchaguzi huo na kutoa taarifa za viashiria vya uvunjifu wa amani.

"Tutaendelea kuwa waadilifu na wazalendo kwa Taifa letu, vijana hatutakengeuka bali tutakua pamoja daima kudumisha umoja na amani ya nchi yetu," alisema Mtilabu.

Wakati wa kongamano hilo, wavyuo hao walipata elimu ya afya kutoka Shirika la Mega We Care dhidi ya UKIMWI, afya ya uzazi na matumizi sahihi ya dawa.



# Tume yaagiza wakulima tumbaku wasajiliwe kielektroniki

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

VYAMA vya Msingi vya Wakulima wa Tumbaku nchini (AMCOS), vimeagizwa kuwasajili wanachama wao kwa mfumo wa kadi za kielektroniki ili kudhibiti udanganyifu na wizuzi wakati wa mauzo.

Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika nchini (TCDC), Dk. Benson Ndiege alitoa agizo hilo wakati akikabidhi magari mawili yaliyonunuliwa na Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima wa Tumbaku Wilaya ya Chunya (CHUTCU).

Ndeige, alisema vyama vingi vya msingi wanachama wake hawajasajiliwa na hawatambuliki kwenye mfumo wa kielektroniki hali ambayo inasababisha kuwepo udanganyifu wakati wa kuuza mazao yao na kusababisha madeni.

Alivitaka vyama hivyo kushirikiana na warajisi wasaidizi kuwasajili wakulima na kuwapatia kadi ambazo zitatumika kuwatambua na kudhibiti utoroshaji wa mazao.

Ndeige, alisema udanganyifu unaofanywa na wakulima unavisababishia vyama hivyo madeni kwenye taasisi za fedha na benki zinakopesha pembejeo za kilimo na ujenzi wa miundombinu.

Aliwashauri viongozi wa AMCOS kuwatumia wahitimu vyuo vikuu na vijana ambao hawana ajira kuwasajili wakulima kwenye mfumo huo ambao utakuwa suluhu ya kudumu ya udanganyifu.

**Ndeige, alisema udanganyifu unaofanywa na wakulima unavisababishia vyama hivyo madeni kwenye taasisi za fedha na benki zinakopesha pembejeo za kilimo na ujenzi wa mi-**

Meneja Uendeshaji wa CHUTCU, Juma Nshinshi, alisema magari hayo yamegharimu zaidi ya Sh. milioni.400 kutokana na mapato ya ndani ya chama hicho.

Nshinshi, alisema bodi ya chama hicho, ilipeleka wazo la ununuzi wa magari hayo kwa wanachama kwenye mkutano mkuu na kuridhia ili kurahisha usafiri wa kuwafikia wakulima kwenye maeneo yao.

Alisema AMCOS ambazo ni wanachama wa CHUTCU zaidi ya 18 na nyingi ziko maeneo ya vijijini, hivyo kuhitaji kuwa na magari yenye ubora ili kuzifikia.

Mwenyekiti wa Bodi ya CHUTCU, Sebastian Masika, alisema ununuzi wa magari hayo utamaliza uhaba wa vyombo vya usafiri.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Chunya, Anakleth Michombero, aliwapongeza viongozi wa CHUTCU kwa kusimamia mali za chama hicho.



Katibu Mkuu wa Chama cha ACT Wazalendo, Ado Shaibu (katikati), akiwanadi wagombea uenyekiti wa vijiji na vitongoji katika vijiji vya Hasamba, Mpemba, Halungu na Igamba, wakati wa uzinduzi wa kampeni za chama hicho, ambao ulihusisha majimbo ya Tunduma, Vwawa na Mbozi, mkoani Songwe, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watalii kwenye mashamba ya chai

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANANCHI wameshauriwa kujenga utamaduni wa kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo kwenye maeneo yao ili kuchochea maendeleo ya sekta ya utalii na kulinda rasilimali za taifa.

Wito huo ulitolewa juzi na baadhi ya wageni wa utalii kutoka nchini Ujerumani akiwemo Werner Schurter waliotembelea Mkoa wa Njombe kwa lengo la kujifunza kuhusu utalii wa kilimo cha chai.

Schurter, alisema amevutiwa na kilimo cha chai na hali ya hewa ya mkoani Njombe na kuwataka wananchi kuona fursa ya kutembelea vivutio na kujifunza.

"Sio mara yangu ya kwanza kuja Tanzania, ninaipenda sana hii nchi, nimefanya kazi hapa lakini sikugundua kama Kusini mwa Tanzania kuna mazingira mazuri hivi," alisema na kusisitiza kuwa: "Mkoa wa Njombe wanatakiwa wajivunie pia kwa mazao walionayo."

Kwa upande wao, wadau wa utalii wa mkoa huo, akiwemo Mkurugenzi wa Kampuni ya Ramika Safaris and Tours, Michael Katona, alisema ujio wa wageni hao ni ishara ya mafanikio katika juhudi za kukuza utalii wa ndani na kimataifa.

Katona, alisema Njombe una fursa kubwa za utalii zinazoweza kuleta manufaa makubwa kiuchumi.

"Leo tumefanya utalii wa kilimo kwa kutembelea mashamba ya chai Kibena na moja ya vitu walivyovutiwa wageni wetu ni pamoja na namna majani ya chai yanavyopatikana kuanzia shambani mpaka kiwandani, kwa kweli tunaona furaha kuwa na sisi tunaweza kuhamasisha wenyeji na wageni kutembelea vivutio vyetu," alisema.

Baadhi ya wakazi wa mjini hapa, akiwemo James Mwakakula, alisema ujio watalii hao unatoa fursa ya kutangaza mkoa kimataifa na kuleta fursa za kiuchumi kwa wenyeji.

# Wanawake wahamasishwa kuwania udiwani, ubunge

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANAWAKE mkoani hapa wametakiwa kugombea udiwani na ubunge katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

Wito huo ulitolewa juzi na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Taifa na Mlezi wa Mkoa wa Njombe, Halima Mohamed Mamuya wakati akizindua Kampeni za Uchaguzi wa serikali za mitaa kimkoa uliofanyika Mtaa wa Kambarage mjini hapa.

Halima, alisema wanawake wanapaswa kuongezeka kwenye nafasi hizo na kuwa wengi katika vyombo vinavyotoa maamuzi.

"Kama jinsi wanawake walivyo wengi kuliko wanaume katika nchi hii, wawe vilevile wengi katika vyombo vinavyotoa maamuzi," alisema na kuongeza kuwa:

" Wanawake hawashindani na wanaume, wanawake ni washirika wa wanaume kwa sababu bila ya mwanamke hakuna mwanaume na bila ya mwanaume hakuna mwanamke."

Asema CCM kinafanya kazi ya kuhakikisha kinaondoa changamoto zinazowakabili wananchi.

"Njombe wameridhika sana kiasi kwamba mitaa 22 imepita bila ya kupingwa kwa sababu wameona huko hata kuonyesha changamoto hakuwezekani maana hazipo," alisema Halima.

Alisema kufuatia mambo makubwa yaliyofanywa na serikali, wananchi wanapaswa kukiamini CCM kwa sababu ndiyo pekee kinaweza kuwaletea maendeleo.

Awali Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Njombe, Justine Nusulupila, alisema chama hicho katika uchaguzi wa serikali za mitaa wametoa kipaumbele kwa wanawake kugombea nafasi ya mwenyekiti.

Mbunge wa Njombe (CCM), Deo Mwanyika, aliwataka wagombea wa chama hicho kutembelea kifua mbele kunadi sera kwa sababu Rais samia Suluhu Hassan amepeleka fedha za miradi katika kila sekta kwenye mitaa na vijiji.

Mbunge wa Lupembe (CCM), Edwin Swalle, aliwataka wananchi kuchagua viongozi wanaotokana na CCM kwa sababu chama hicho kimetekeleza vema Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020-2025 kwa kuboresha sekta za elimu, afya, maji, barabara, kilimo na viwanda.

# 'Msisuse uchaguzi wa kuchagua viongozi wa mitaa'

**Na Mwandishi Wetu,** NJOMBE

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimewataka wananchi mkoani hapa kujitokeza kwa wingi kwenda kuchagua viongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika Novemba 27, mwaka huu na kutimiza haki yao kikatiba.

Wito huo ulitolewa juzi na Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Magharibi, Dickson Matata wakati akizindua kampeni za chama hicho katika Kata ya Ramadhani mjini hapa.

Matata, alisema wananchi hao wanapaswa kujitokeza kwenda kupiga kura na kuchagua viongozi wa chama hicho na sio kususia uchaguzi huo kwa sababu kufanya hivyo ni kujinyima haki yao ya msingi na kukosa maendeleo katika maeneo yao kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Katibu wa CHADEMA Kanda ya Kati, Emmanuel Masonga, aliwahamasisha wananchi kujitokeza kwenda kushiriki uchaguzi ili kuweka mustakabali wa kipindi hicho cha miaka mitano ijayo kwa kuchagua viongozi bora.

Masonga, alisema wananchi hao wanatakiwa kuwa makini kwa kuchagua viongozi wanaowaamini, sio wanyanyasaji na wenye roho za kikatili.



# ZEC kuandikisha wapigakura wapya 78,000 mwakani

## -Yatangaza mabadiliko mipaka majimbo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TUME ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) inatarajia kuandikisha wapiga kura wapya zaidi ya 78,000 katika awamu ya pili ya uboreshaji wa daftari la wapigakura kuanzia Februari mwakani ili nao washiriki kuchagua viongozi katika Uchaguzi Mkuu 2025.

ZEC inarejea uandikishaji wapiga kura hao baada ya kutimiza umri wa miaka 18 mwaka huu katika awamu hiyo kwa kuwa ni haki yao ya kikatiba kuchagua viongozi wanaowataka kwa ajili ya kuwaletea maendeleo.

Hatua hiyo inakuja baada ya kukamilisha zoezi hilo kwa awamu ya kwanza Januari 15, mwaka huu, ikiwa ni maandalizi ya uchaguzi huo wa mwaka 2025, utakaovishirikisha vyama vingi vya siasa.

Katika awamu hiyo ya kwanza, jumla ya wapigakura wapya 57,883 waliandikishwa katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari visiwani hapa jana, Mwenyekiti wa ZEC, Jaji George Kazi, alisema awamu hiyo ya pili ya uandikishaji wapiga kura, itaanza Februari 1, mwakani katika Wilaya ya Micheweni na kuhitimishwa Machi 17, mwakani Wilaya ya Mjini.

Kazi, alisema uandikishaji huo utafanyika katika vituo vyote 407 kwa muda wa siku tatu kwa kila shehia ya visiwa hivyo.

Alisema kwa mujibu wa Takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, ZEC inatarajia kuandikisha wapigakura wapya 78,922 waliotimiza umri wa miaka 18 kwa mwaka huu.

Kazi, alisema wengine watakaoandikishwa ni wale ambao hawajawahi kuandikishwa katika daftari hilo tangu lianzishwe nchini.

Alisema tume hiyo kupitia ofisi zake za wilaya, inaendelea kutoa huduma za kuhamisha taarifa za wapigakura, kusahihisha na kupokea maombi ya kufuta taarifa za waliokosa sifa.

"Zoezi hili linafanyika kila siku za kazi katika ofisi zetu za ZEC za wilaya katika wilaya zote 11 Unguja na Pemba," alisisitiza Kazi

> **"Zoezi hili linafanyika kila siku za kazi katika ofisi zetu za ZEC za wilaya katika wilaya zote 11 Unguja na Pemba," alisisitiza Kazi**

Aliwataka wananchi wenye sifa kujitokeza kujitokeza kujiandikisha katika maeneo yao wakati utakapofika ili waweze kushiriki katika uchaguzi huo na kuchagua viongozi bora watakaowaletea maendeleo.

"Awamu hii ya pili ni uandikishaji wa mwisho kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, hivyo naamini wananchi watajitayarisha na uandikishaji huu na kujitokeza kwa wingi kupata haki yao msingi ya kupiga kura," alisema Kazi.

**MAREKEBISHO MIPAKA**

Wakati huo huo; ZEC imefanya marekebisho madogo ya mipaka ya majimbo ya Wete na Mtambwe kisiwani Pemba.

Kazi amesema ZEC imelazimika kufanya hivyo kufuatia mabadiliko ya wadi yaliyofanywa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum.

Mabadiliko hayo ni kuihamisha Shehia ya Limbani katika Jimbo la Wete na Shehia ya Mzambarau Jimbo la Mtamwe.

Majimbo hayo yalitangazwa katika gazeti rasmi la Serikali kupitia tangazo la kisheria namba 108 ya mwaka 2020 la Agosti 28, mwaka 2020.

Mabadiliko hayo yanahusisha Shehia ya Limbani ambayo awali ilikuwa Wadi ya Piki Jimbo la Mtambwe na sasa itasomeka Shehia ya Limbani Wadi ya Jadida Jimbo la Wete.

Shehia ya Mzambarau katika Wadi ya Pandani Jimbo la Pandani itasomeka katika Wadi ya Piki Jimbo la Mtambwe.

Hata hivyo, Kazi, alisema kuelekea uchaguzi huo, ZEC haitachunguza idadi ya mipaka na majina ya majimbo na badala yake yatabaki kama yalivyokuwa katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.



Wajasiriamali wakionesha bidhaa mbalimbali wanazozalisha kwenye mkutano uliowakutanisha wajasiriamali, serikali, pamoja na wadau kupitia Jukwaa la Panda 2024, katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, mapema wiki hii. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# IMAS mwarobaini urasimu mikopo wajasiriamali

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mtendaji Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi nchini (NEEC), Beng'i Issa amesema Programu ya Imarisha Uchumi na Mama Samia (IMAS) itaondoa changamoto na urasimu wa upatikanaji wa mikopo kwa wananchi nchini na kuwawezesha kujikwamua na umaskini. Akizungumza juzi na waandishi wa habari baada ya kutoa mafunzo kwa wakazi wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Issa alisema serikali inatumia mifumo ya kidigitali kurahisisha upatikanaji wa mikopo kwa wananchi, hivyo ni vyema wakapewa elimu ya kuifahamu ili kupata mikopo inayotolewa na programu hiyo.

Alisema programu hiyo itaboresha uchumi wa mtu mmoja mmoja baada ya kupatiwa ujuzi na kuoneshwa fursa ambazo serikali imetenga.

"Katika programu ya IMASA kwa hapa Zanzibar tumegundua hakuna tatizo la mitaji, mitaji ipo, serikali imetoa fedha, tatizo kubwa lipo kwenye ufahamu wa watu jinsi gani ya kupata mitaji, upatikanaji wa taarifa na vigezo vinavyotakiwa ili aweze kupata mkopo" alisema Issa. Akifungua mafunzo hayo, Mkuu wa Mkoa huo, Idrissa Kitwana Mustafa, alisema ni fursa ya pekee kuhakikisha makundi mbalimbali yanapata fursa ya kiuchumi kupitia mikopo inayotolewa na serikali.

Mustafa, alisema mikopo hiyo ina lengo la kuwasaidia wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo kufikia malengo yao ya kujikomboa kiuchumi na kuondokana na umasikini.

Mshauri wa Rais Samia katika masuala ya wanawake, wazee na makundi maalum ya watu wenye ulemavu, Sophia Mjema, aliwataja wajasiriamali kuchangamkia fursa hizo na kuondokana na umaskini

Mjema, alisema uhakiki wa IMASA kwa nchi nzima kwa awamu ya kwanza umefikia asilimia 80 kwa uandikishaji.

Alisema wananchi wengi wamefurika katika mikutano ya utoaji wa elimu ya jinsi ya upatikanaji wa fursa za mikopo ya kuanzisha miradi ya ujasiriamali nchini.

Mkurugenzi wa Wakala Uwezeshaji Zanzibar (ZEA), Juma Burhan, alisema lengo kuu ni kwenda kidigitali kuomba mikopo. Kwa mujibu wa Burhan, ndani ya siku 14 mwombaji anapata mkopo inayookana na program hiyo baada ya kukidhi vigezo

Alisema ZEA imetoa mkopo ya shilingi milioni 18 kwa mkoa huo, fedha ambazo zinatokana na Uviko- 19 baada ya serikali kutenga kuwawezesha wajasiriamali. Alisema Mkoa wa Mjini ndio ambao umezalisha ajira nyingi kupitia fedha hizo.

Mjasiriamali, Mtumwa Soud, aliwatata wanawake wenzake kuchangamkia fursa hiyo kwa ajili ya kuendeleza biashara zao.

# UVIDA janga kwa binadamu, mimea

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imesema usugu wa Vimelea vya Maradhi dhidi ya Dawa (UVIDA) ni janga kwa uchumi na afya ya mwanadamu, wanyama, mimea na mazingira duniani.

Hayo yamo katika taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa jana Waziri wa Wizara hiyo, Nassor Ahmed Mazrui kuhusiana na janga hilo la UVIDA linaloinyemelea jamii

Mazrui alifafanua kuwa UVIDA ni hali ya vimelea vya magonjwa kustahimili nguvu ya dawa kuua vimelea hivyo na kutibu magonjwa.

Alivitaja vimelea hivyo kuwa ni bakteria, fangazi na virusi kubadilika na kuwa sugu kwa dawa zilizokusudiwa kwa matibabu ya mgonjwa.

Alisema vidudu hivyo hupelekea kuchelewa kupona kwa maradhi, mgonjwa kukaa hospitali muda mrefu, ongezeko la gharama za matibabu na kushuka kwa pato la taifa.

Waziri huyo, alisema takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), zinaonyesha takriban vifo milioni tano husababishwa na UVIDA kila mwaka na kuwa chanzo cha tatu cha vifo vyote vilivyoripotiwa ulimwenguni kutokana na maradhi yote.

"Ukiacha Kifua Kikuu (TB), UKIMWI (Upungufu wa Kinga Mwilini) na Malaria ambavyo vimeshika nafasi ya 10, 11 na 12 kwa kufuatana. Kwa Tanzania ripoti ya mwaka 2019 inaonesha takribani vifo 66,500 vilitokana au kuchagizwa na UVIDA, " alisema Mazrui.

Alisema kwa upande wa Zanzibar, serikali ya Zanzibar imechukua hatua za kupambana na janga hilo ikiwemo kuandaa mpango mkakati wa kisekta wa UVIDA.

Mazrui, alisema mpango mkakati huo umelenga kutoa elimu kwa jamii, kufanya tafiti, ukusanyaji wa taarifa, kuzuia kuenea vimelea vya magonjwa na kusimamia matumizi sahihi ya dawa.

Alisema wizara hiyo na wadau wanahitaji kutumia Jukwaa la Afya Jumuishi kukabiliana na UVIDA dhidi ya afya ya binadamu, wanyama, mimea na mazingira.

Alisema ubora huo utapatikana kwa kusimamia matumizi sahihi wa dawa hasa za antibiotiki kwa kuhakikisha mgonjwa anamaliza dozi kwa wakati sahihi.

Vilevile kufuata maelekezo ya watalamu wa mifugo na kilimo juu ya matumizi sahihi ya dawa kwa mifugo na mimea na kunawa mikono mara kwa mara kwa sabuni na maji tiririka hasa baada ya mtu kutoka chooni, kabla na baada ya kula.

Alisema nyingine ni kuhakikisha wananchi wanapata chanjo za maradhi ya kuambukiza na kwa wanyama, madaktari kuandika dawa ya kuua (sumu) mara kwa mara baada ya kujiridhisha kwa kufanya vipimo.

Alisem wafamasia nao wanatakiwa wasitoe dawa ya kuua (sumu) bila cheti cha daktari na watoe maelekezo ya kutumia dawa kwa usahihi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**SELEMAN ABBAS GHULIKU,** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili MC 450 CJH. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi:

**PHQ/DAR/KIN/251921/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MOHAMEDASLAM ABDULAZIZ BARDE** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T.348 ADW aina ya Toyota HIACE. Yenye umiliki wa jina la AL-HILAL CHARITABLE DISPENSARY Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya polisi;

**PHQ/DAR/ILA/255621/2024.**

**FORM 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 26102 OF 2024**
**In the Matter of Estate of the Late**
**TAHERALI RAJBHAI YUSUFALI**
**And**
**In the Matter of Application for letters of administration by**
**ZAKIYUDIN TAHERALI RAJBHAI**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above -named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 12 day of DEC 2024
Dated at DAR ES SALAAM this 19th day of NOV 2024

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LUCY ENGELS MRIKARIA**

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 794 CCP aina ya NOAH. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi:

**PHQ/DAR/ILA/256970/2024.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**FRANK MASANJA MAGANGA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index No. **S1845/0063** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **SEEKE SECONDARY SCHOOL** mwaka 2018, Cheti cha kidato cha sita chenye index No. S1129/0589 Kilchotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **IGUGUNO SECONDARY SCHOOL** mwaka 2021. Vyeti hivi vimepotea Jijini **DODOMA.** Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.Taarifa ya Polisi:**PHQ/DOD/DOD/5331/2023** Taarifa ya Polisi : **PHQ/DOD/DOD/5333/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Wilaya ya CHEMBA**
**Kituo cha CHEMBA Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa Mirathi Na 28339/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU TERESIA AKWESU LAGU WA CHEMBA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA MARSELI BAHA MCHUNO**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, Wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 19 Mwezi 12 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
*Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa.
* Marehemu hakuacha Wosia
*Futa isiyohusika
**Imetolewa leo tarehe 18 Mwezi 11 Mwaka 2024**

**HAKIMU**

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI

**WILBARD PETER MRIMA**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaji yenye namba za usajili MC 712 DQB Chasses Namba MD6M14PABN4B79382, Engine Namba AK4BN4798491. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . Polisi Taarifa :

**PHQ/ KIL/MOS/28293/2024**

**Summons to appear (O.V, R.20 (1) of (CPC)**
**(Substituted Service)**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**
**MISC.LAND APPLICATION NO. 26146 OF 2024**
**ZAINA MOHAMEDI GOMA & ANOTHER ......APPLICANTS**
**VERSUS**
**THE ATTORNEY GENERAL & 8 OTHER ........ RESPONDENTS**
**TO**

- **JULIAN SHAWN KADRI ( As administrator of Estate Late OMARI KADRI BAKSH)**

**MLANDIZI – KIBAHA**

- **ADILI AUCTION MART P.O. BOX 4061**
- **CHRISMILI FARM LIMITED**

**MLANDIZI – KIBAHA**
**WHEREAS:** The above named APPLICANT has Institute the SUIT against you, you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or authorized Agent on 05th day of DECEMBER 2024 at 10; 00 PM for MENTION Before Hon. N.E. MANDIA, Judge to answer the said SUIT and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to reply in support of your reply.
TAKE NOTICE that in default of your appearance on that day, the said matter will be heard and determined in your absence.
Given under my hand and the seal of this Court, this 19th day of NOVEMBER 2024.

**DEPUTY REGISTRAR**

## TANGAZO LA KUPOTELEWA NA NYARAKA UMILIKI WA KIWANJA

**ASIA HAMIDU DAVID**

Anatangaza kupotelewa na nyaraka ya umiliki wa kiwanja namba 527 kitalu "JJ" Ndembezi Manispaa ya Shinyanga. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu.Taarifa ya polisi:

**PHQ/SHI/SHI/11389/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Moshi**
**Kituo cha Moshi Mjini Mkoa Kilimanjaro.**
**Shauri la Madai 169, 2024.**
**Jina la Mdai JOEL ERNEST**
**Jina la Mdaiwa JEROME JUDIKA KIMARO.**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Kwa: JEROME JUDIKA KIMARO.**
**Kwa kuwa Madai/Wadai ameleta /Wameleta madai yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai)**

Fika Mahakamani kujibu madai ya Tsh 3,614,000/= dhidi yako yaliyotokana na biashara ya maziwa mliyoingia na mdai mnamo 14/08/2023.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 22 mwezi 11 mwaka 2024 saa 07:00 mchana kwa mujibu wa maombi hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashaidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya w ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 12 mwezi 11 Mwaka 2024

.....................
**HAKIMU**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA DODOMA**
**SHAURI LA ARDHI NA. 27265/ 2024**
**JOYCE HARUN MACHODO............ MWOMBAJI**
**DHIDI YA**

- **TANZANIA COMMERCIAL BANK(TCB) PLC ...MJIBU MAOMBI**
- **PATRICK EMMANUEL RUGEZI.........MJIBU MAOMBI**
- **AGNESS AMOS MPAMBIJE.........MJIBU MAOMBI**
- **THE ATTORNEY GENERAL.........MJIBU MAOMBI**

**KWA: TANZANIA COMMERCIAL BANK (TCB) PLC**
**PATRICK EMMANUEL RUGENZI**
**AGNESS AMOS MPAMBIJE**
**POPOTE PALE MLIPO**
**YAH: TAARIFA YA KUSIKILIZWA KWA SHAURI LA ARDHI NA. 6735/ 2024**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA.**
MNAFAHAMISHWA KWAMBA; Shauri tajwa hapo juu litasikilizwa Mahakama kuu Tanzania, kanda ya Dodoma, mbele ya Mhe. Jaji I. D. MUSOKWA, wa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma, saa tatu kamili (9:00) asubuhi siku ya Jumanne tarehe 10/12/2024.
HIVYO BASI; mnatakiwa mfike mwenyewe au Wakili wenu siku hiyo iliyotajwa bila kukosa .
NA ENDAPO; hamtofika mwenyewe au mawakili wenu siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakavyoamua pasipo nyie au mawakili wenu kuwepo.
IMETOLEWA; Kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 12 mwezi wa Novemba, 2024.

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DODOMA**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**NASSOR SEIF SAAD** anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria yenye namba TAE 311898 .Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/223512/2024.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**SELEMAN ABBAS GHULIKU,** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili MC 450 CJH. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi:

**PHQ/DAR/KIN/251921/2024.**

## TANGAZO LA KUPOTELEWA NA NYARAKA UMILIKI WA KIWANJA

**THECLA ANDREW TIBANDEBAGE** anatangaza kupotelewa na nyaraka ya umiliki wa kiwanja namba 757 kitalu "PP" Mwadui Shinyanga Manispaa. Kwa yeyeto atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu Taarifa ya polisi:

**PHQ/SHI/SHI/11391/2024**

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku
Piga Simu 0677020701

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Idadi kubwa ya watu wahofiwa kufa Gaza

**GAZA,** Palestina

MAOFISA katika hiospitali moja iliyoko kaskazini mwa Gaza wanasema watu wengi wanahofiwa kuuawa katika mashambulizi ya anga ya kutisha yaliyofanywa na Israel usiku wa kuamkia jana.

Hata hivyo, vikosi vya uokoaji vya Gaza vilisema shughuli za kuwanasua watu waliokwama kwenye vifusi zilianza mapema asubuhi.

Mashambulizi ya anga ya Israel yalilenga majengo matano katika eneo la Beit Lahia na jiji la Gaza.

Vyombo vya habari vinavyohusiana na Hamas vilisema makumi ya watu waliuawa, huku idadi kubwa ya watu wamefukiwa kwenye vifusi.

Hakuna kauli kutoka kwa jeshi la Israel hadi sasa. Lakini hivi karibuni jeshi la nchi hiyo limezidisha mashambulizi yake kaskazini mwa Gaza, ikielezwa inawazuia Hamas kujipanga upya.

Maeneo ya kaskazini mwa Gaza yako chini ya mzingiro wa majeshi ya Israel na hakuna msaada wa kibinadamu ambao umetolewa kwa muda wa siku 40, kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa.

Madaktari wa Gaza walisema wanapata shida kuwatibu waliojeruhiwa kutokana na kukosa madawa na vifaa tiba.

Mapema wiki hii, takriban watu 34 waliuawa katika shambulio la anga la Israel kwenye jengo la ghorofa tano la makazi katika eneo la Beit Lahia.

Shirika hilo lililonukuliwa na shirika la habari la AFP, lilisema wengi wa waliofariki ni wanawake na watoto.

Mashambulizi ya ardhini ya Israel kaskazini mwa Gaza yamesababisha watu 130,000 kukimbia makazi yao katika muda wa wiki tano zilizopita.

Umoja wa Mataifa ulisema watu 75,000 wamebaki katika eneo hilo ambalo liko chini ya mzingiro, huku kukiwa na uhaba wa maji na chakula. **BBC**





Wanajeshi wa Russia wakiwa na makombora ya kuvuka mabara aina ya Topol-M, hivi karibuni.**PICHA: ALLIANCE**

# Russia yaanza ubabe

**MOSCOW,** Russia

- Yaipiga Ukraine kwa bomu zito
- Ulaya yaimarisha ulinzi kujilinda

SIKU mbili baada ya Marekani kuiruhusu kwa mara ya kwanza Ukraine kutumia makombora yake ya masafa marefu na jana Uingereza imefuata mkondo huo, Russia imejibu vikali hatua hiyo kwa kurusha kombora kubwa la kuvuka mabara kuishambulia Ukraine.

Kutumika kwa kombora hilo kubwa na lenye nguvu zaidi, kumeibua hofu kwa mataifa jirani na yale ya Ulaya ambayo yameanza kuchukua hatua mbalimbali za kujilinda.

Makombora ya masafa marefu ya Marekani na Uingereza yalitumiwa na Ukraine kushambulia maeneo tofauti yaliyo ndani ya ardhi ya Russia juzi na jana.

Russia ilifyatua kombora la kuvuka mabara jana kutokea mkoa wake wa kusini wa Astrakhan, na kuishambulia Ukraine.

Hiyo ni mara ya kwanza kwa nchi hiyo kutumia silaha zenye nguvu kubwa namna hiyo tangu ilipoanzisha vita hivyo.

Jeshi la anga la Ukraine lilitoa ripoti ikisema kwamba shambulio hilo limeilenga miundo mbinu kadhaa muhimu katika mji wa Dnipro.

Shambulio hilo la Russia linashuhudiwa ikiwa ni baada ya Ukraine nayo kushambulia kwa mara ya kwanza kutumia makombora yaliyotoka Marekani na Uingereza.

Hatua hiyo ya Russia inatokana na onyo ililotoa miezi kadhaa nyuma, ikionya Ukraine kwamba itazidisha makali kwenye vita hivyo.

Haijakuwa wazi kutoka Ukraine kuhusu uharibifu uliofanywa na shambulio hilo la jana kutoka Russia la kombora la masafa marefu.

Lakini pia Urusi kupitia msemaji wake wa wizara ya mambo ya nje Maria Zakharova, alisema iko tayari kutafakari juhudi zozote za kweli za kuleta amani katika mgogoro huo na ambazo zitazingatia maslahi yake na hali halisi ya vita hivyo, lakini sio juhudi zenye mirengo ya kisiasa.

Marekani ilitangaza Jumatano inataka kuipelekea Ukraine mabomu ya kutega ardhini ili kuisaidia nchi hiyo kuvirudisha nyuma vikosi vya Urusi.

Hata hivyo, kumekuwa na ukosoaji kutoka shirika la kutetea haki za binadamu la Human rights Watch kutokana na athari zinazoweza kusababishwa na mabomu hayo kwa raia .

Kufuatia hali inayoendelea hivi sasa kwenye vita hiyo, Hungary iilisema itaweka mfumo wa ulinzi wa anga katika eneo lake la Kaskazini Mashariki kutokana na kitisho cha kutanuka kwa vita kwa namna ambayo haijawahi kutokea.

Waziri wa Ulinzi wa nchi hiyo, Kristof Szalay- Bobrovniczky alisema bado wanaamini amani inaweza kupatikana hivi karibuni kupitia mchakato wa kidiplomasia na sio wa kijeshi, lakini pia akasisitiza ni bora zaidi kujiandaa kwa lolote linaloweza kutokea.

Uamuzi huo wa Hungary umefanyika baada ya mkutano wa baraza la ulinzi la nchi hiyo uliotishwa na waziri mkuu Viktor Orban, kujadili kinachoendelea katika vita vya Ukraine.

Itakumbukwa kwamba Hungary ni mshirika wa jumuiya ya kujihami ya NATO na pia mwanachama wa Umoja wa Ulaya ambayo inapakana na Ukraine.

Jeshi la nchi hiyo hivi sasa liko kwenye mpango wa kuimarisha uwezo wake huku ikielezwa kwamba baadhi ya vikosi vyake vimeshawekwa katika hali ya tahadhari.

Kwa upande mwingine, mawaziri wa ulinzi wa mataifa ya Jumuiya ya kanda ya Kusini Mashariki mwa Asia-ASEAN walikutana jana na naibu waziri wa ulinzi wa Korea Kusini Kim Seon, kujadili suala hilo.

Kulingana na Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC), Ukraine, ilianza kurusha makombora ya masafa marefu ambayo yalilenga shabaha ndani ya Russia.

Serikali ya Uingereza ilikataa kutoa maoni yake kuhusu ripoti hizo, lakini maofisa wamethibitisha kwamba Waziri wa Ulinzi, John Healey, alizungumza na waziri mwenzake wa Ukraine , inahofia huenda walijadili suala hilo.

Mawaziri hao walichukua tahadhari katika majibu yao kwa ripoti hizo kutokana na wasi wasi juu ya majibu ya Russia, pamoja na kuhakikisha hatua hiyo haionekani kuwa inaongozwa na Uingereza.

Waziri wa Ulinzi wa Ukraine, Rustem Umerov pia alikataa kuthibitisha kwamba nchi yake imetumia makombora ya Storm Shadow kushambulia ndani ya ardhi ya Russia, lakini alisema tunatumia njia zote kuilinda nchi yetu.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani, Matthew Miller, aliambia BBC ikiwa Ukraine inashauriana au kuifahamisha Marekani kuhusu matumizi ya makombora yaliyotolewa na Uingereza.

Alisema hatazungumza hadharani kuhusu matumizi ya silaha za nchi nyingine.

Rais Volodymyr Zelensky ametoa wito mara kwa mara kwa washirika wake wa Magharibi kuidhinisha matumizi ya makombora ya masafa marefu dhidi ya shabaha za ndani ya Russia, akisema ndiyo njia pekee ya kukomesha vita.

Kombora la Storm Shadow linachukuliwa kuwa silaha bora ya kupenya mahandaki magumu na ghala za silaha, kama makombora yanayotumiwa na Russia katika vita yake dhidi ya Ukraine.**BBC**

# SINGIDA YATAKA KUMSAJILI CHASAMBI, NKANE DESEMBA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Singida Black Stars imeanza kumnyemelea winga wa Simba, Ladack Chasambi, ili kumnasa katika dirisha dogo la usajili linalotarajiwa kufunguliwa ifikapo Desemba 15, mwaka huu.

**Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema Kocha Mkuu wa Singida Black Stars, Patrick Aussems, amewaambia mabosi wa timu yake anamhitaji kijana huyo kwa ajili ya kukiongezea nguvu kikosi chake.**

Chanzo chetu kinasema Aussems anaamini ili kuendelea kupambana kuwania taji la ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara au kumaliza katika nafasi nne za juu, atalazimika apate wachezaji wazuri zaidi kwenye kikosi chake.

Mtoa taarifa alisema kocha huyo anaonekana kumhusudu winga huyo ambaye ameonekana hapati nafasi sana katika kikosi cha Wekundu wa Msimbazi kwa sasa.

"Kingine ambacho tunaona tunaweza kufanikiwa kumpata, kwa kumsajili au ikishindikana sana hata kwa mkopo ni ujuzi wa Elie Mpanzu, yule ni winga, amekuja kuongeza ugumu kabisa katika kikosi cha Simba, kwa maana hiyo tunaweza kufanikiwa kwa hilo," kilisema chanzo chetu.

Tayari Simba imemsajili Mpanzu, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo), ambaye kwa sasa anasubiri kufunguliwa kwa dirisha hilo ili kuanza kazi na kikosi hicho.

Chasambi alisajiliwa na Simba dirisha dogo la usajili msimu uliopita akitokea Mtibwa Sugar, ambapo pamoja na kufanya vyema pindi anapopata nafasi finyu ya kucheza, lakini amekuwa akipata tabu hata kuingia kipindi cha pili, achilia mbali kuanza, mbele ya mawinga wenzake kikosini hapo kama Kibu Denis, Edwin Balua, Joshua Mutale na wengine.

Taarifa pia kutoka ndani ya Singida Black Stars zinasema huenda wakafikiria pia kumchukua, Denis Nkane wa Yanga, ingawa Aussems hajasema lolote kuhusu mchezaji huyo.

"Kuna mchakato viongozi wetu wameanza kwa ajili ya kutaka kuongeza upana wa kikosi. Tunajua ushindani ni mkubwa na ni lazima kila idara iwe imara," aliongeza mtoa habari wetu.

Singida Black Stars imeanza mkakati wa kutaka kukiimarisha kikosi chake wakati ikiwa ni moja ya timu zilizoonyesha ushindani katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara inayotarajiwa kuendelea leo kwa Pamba Jiji kuwakaribisha vinara wa ligi, Simba.

Katika msimamo wa ligi hiyo, Singida Black Stars iko kwenye nafasi ya tatu ikiwa na pointi 23 baada ya kucheza michezo 10 sawa na Simba yenye pointi 25 huku mabingwa watetezi, Yanga wakiwa na pointi 24.

## *JKU yadai bado hawajapoteza matumaini*

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BAADA ya kulazimishwa sare na Kipanga, benchi la ufundi la JKU SC limesema bado wanaamini watatetea ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar ambao wanaushikilia, imeelezwa.

JKU imetoka sare ya bao 1-1 na Kipanga katika mechi ya raundi ya 12 iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mau A juzi jioni.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa JKU SC, Mselem Sultani, alisema kuna utofauti wa alama tisa kati yao na vinara wa ligi hiyo Mafunzo, hivyo wataendelea kupambana kuhakikisha wanapata ushindi michezo inayofuata.

Sultani alisema kufanya vibaya kwa timu yake haimaanishi tayari wamepoteza nafasi ya kubeba taji hilo katika msimu huu unaoendelea.

"Tunayo nafasi ya kurekebisha makosa katika michezo mitatu iliyobaki ya mzunguko wa kwanza na hata michezo yote ya mzunguko wa pili tutakayocheza.

Bado tupo katika hizo mbio za ubingwa, na kulingana na ligi ilivyo tunayo nafasi ya kutetea taji letu kwa msimu huu, tutarudi katika uwanja wa mazoezi na kuendelea kukifanyia maboresho kikosi chetu,"Sultani alisema.

Kocha huyo amewaomba viongozi wa Bodi ya Ligi na Kamati ya Waamuzi kuwaangalia kwa 'karibu' waamuzi baada ya kuwakabidhi majukumu ya kusimamia michezo ya ligi.



Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro (mwenye shati jeupe), akishangilia baada ya Timu ya Soka ya Tanzania (Taifa Stars), kufuzu kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2025), zitakazofanyika mwakani nchini Morocco. Stars ilipata nafasi hiyo baada ya kuifunga Guinea bao 1-0. **PICHA: TFF**

## Wachina kutumia filamu kuibeba TZ

**Na Restuta James**

BAADHI ya wadau wa utamaduni kutoka Tanzania na China, wamesema mabadilishano ya kitamaduni kati ya nchi hizo, kupitia vipindi vya televisheni, ni nyenzo muhimu ya kujifunza kwa wananchi wa pande zote.

Wadau hao walitoa maoni hayo jiini Dar es Salaam hivi karibuni, wakati wa hafla ya uzinduzi wa China Media Group (CMG), itakayorusha filamu za Kichina na vipindi vya watoto vilivyotengenezwa nchini humo, katika chaneli za Tanzania.

Msanii wa filamu, Hugo Fernandez, alisema kuna mfanano mkubwa wa kitamaduni kati ya China na Tanzania, hasa kuimba wakati wa kufanyakazi mashambani.

Fernandez alisema baadhi ya wakulima China, huwa wanaimba wanapokuwa shambani kama inavyofanyika katika maeneo mbalimbali Tanzania, akitolea mfano Wasukuma huimba wanapolima kama inavyofanyika nchini kwao.

"Tunapochunguza zaidi na kujihusisha na mabadilishano haya ya kitamaduni, ndivyo tunavyoweza kujifunza zaidi, kuunda na kuvumbua," alisema Fernandez.

Msanii huyo alibainisha ushirikiano wa kitamaduni unaweza kuibua fursa za kibiashara kwa Jumuiya za Kitanzania, kwa kupata msukumo kutoka katika Filamu za Kichina na kutafuta njia mpya za ushirikiano kupitia ubia wa kibiashara.

"Tunaamini ushirikiano huu utawapa fursa Watanzania na Wachina katika tasnia ya filamu, lakini kila upande utanufaika kwa sababu ya kujifunza kile kinachofanywa na taifa lingine, tunakwenda katika ya kisasa na hivyo ni lazima kwenye kusaka maendeleo, zitumike njia mbalimbali," aliongeza msanii huyo.

Tukio hilo pia liliwapa watengenezaji filamu na wasanii wa Kitanzania fursa ya kuungana na watayarishaji wa kimataifa, na hivyo kufungua mlango wa mikataba na ushirikiano.

Wakili wa Mahakama Kuu, Novatus Igosha, alisema filamu inayoonyesha Wachina wakiwa shambani, itatoa mwanga wa kujifunza kwa wakulima hapa Tanzania kwa sababu kilimo kinagusa idadi kubwa ya wananchi.

Igosha alisema filamu na vipindi vya Kichina vina maudhui yenye staha yanayoweza kutazamwa na familia nzima.

"Mabadilishano ya maadili ya kitamaduni na mawazo ya kiuchumi ni muhimu kwa nchi zote mbili," Igosha aliongeza.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### GYOKERES ATAKIWA MAN

MANCHESTER United wameambiwa kuwa Sporting huenda wakamuuza mshambuliaji wa Sweden, Viktor Gyokeres, 26, lakini sio katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Mirror)***

#### QUENDA NAE KWENYE RADA

KLABU ya Manchester United pia inajaribu kutaka kumnunua winga wa Sporting mwenye umri wa miaka 17, Geovany Quenda raia wa Ureno. ***(A Bola)***

#### SZCZESNY MKATABA MPYA

BARCELONA inafikiria kumpa kipa Wojciech Szczesny, 34, mkataba mpya wiki chache baada ya raia huyo wa Poland kujiunga na klabu hiyo. ***(Marca)***

#### CARLOS KUUZWA JANUARI

KOCHA wa Aston Villa, Unai Emery anaweza kuamua kumuuza mlinzi wa Brazil, Diego Carlos, 31, Januari. ***(Football Insider)***

#### NEYMAR KUREJEA SANTOS

WINGA wa Brazil Neymar, 32, anatazamiwa kurejea Santos huku klabu yake ya Saudi Arabia, Al-Hilal ikifadhaishwa na matatizo ya jeraha la mchezaji huyo. ***(Cesar Luis Merlo)***

#### ORKUN KOKCU AMSIFIA SLOT

KIUNGO wa kati wa Benfica na Uturuki, Orkun Kokcu, 23, amesifu mchango ambao kocha wa Liverpool, Arne Slot amekuwa nao kwenye maisha yake ya soka huku kukiwa na uwezekano wa kuhamia Anfield. ***(Liverpool Echo)***

#### FULHAM YAMTAKA JESUS

KLABU ya Fulham imeingia kwenye kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa kimataifa wa Brazil, Igor Jesus, 23, kutoka Botafogo. ***(TBR Football)***

#### WINKS ATAKIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inaangalia uwezekano wa kumsajili tena kiungo wa kati wa England, Harry Winks, 28, baada ya kumuuza kwa Leicester City mwaka jana. ***(Fichajes)***

#### VLAHOVIC AFUATILIWA

ARSENAL bado inafuatilia hali ya mshambuliaji wa Serbia, Dusan Vlahovic, 24, katika klabu ya Juventus. ***(Rudy Galetti)***

#### YATAKA MSHAMBULIAJI

KLABU ya Crystal Palace ina nia ya kusajili mshambuliaji wakati katika uhamisho wa Januari lakini wana bajeti ndogo. ***(NipeSport)***

#### KVARATSKHELIA KUONDOKA

MASHAMBULIAJI wa Georgia, Khvicha Kvaratskhelia mwenye umri wa miaka 23, anaweza kuondoka Napoli kwa vile mazungumzo yake ya mkataba mpya yamekwama huku Barcelona na PSG zikimtaka. ***(Goal)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BRUNO AFICHUA KUTAKIWA MAN CITY

**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa kati wa Newcastle United, Bruno Guimaraes amefichua alikuwa na mazungumzo na kocha wa Manchester City Pep Guardiola katika kipindi cha majira ya joto kuangalia uwezekano wa kuhamia kwenye klabu hiyo.

Guimaraes alihusishwa kwa kiasi kikubwa kuhamia Man City na Arsenal wakati wa majira ya joto wakati mkataba wake wa Newcastle ulijumuisha kifungu cha kuachiliwa kwa pauni milioni 100, kabla ya mauzo ya Yankuba Minteh na Elliot Anderson.

**Kiungo huyo alimaliza uvumi huo Agosti kwa ujumbe wa hisia uliojadili upatikanaji wake.**

### Kiungo huyo wa Newcastle amesema Guardiola alimuhitaji na kuweka....

Katika mahojiano ya hivi majuzi na Globo Esporte, Guimaraes alithibitisha tena mapenzi yake kwa Newcastle, lakini hakuweza kuficha matamanio ya City kuhitaji huduma yake.

"Ninaamini kuwa katika klabu yangu mimi nina heshima kubwa.

"Mimi ni nahodha wa Newcastle na ni kitu ambacho kama ungeniuliza miaka mitatu iliyopita, ndoto yangu kubwa ingekuwa kucheza Ligi Kuu England na kuichezea. Naipenda sana Newcastle .

"Ni kweli, kuwa na nia ya Manchester City inaonesha niko kwenye kiwango cha juu, lakini haikuwa kitu zaidi ya maslahi.

"Najua Guardiola anapenda soka langu, ni kawaida kuwa na makocha wakubwa wanaopenda soka lako. Tumezungumza mara baada ya mahojiano, nilisifu kazi yake, alisifu kazi yangu, lakini haikuwa zaidi ya hiyo."

Mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 utaendelea hadi 2028 na kuipa Newcastle udhibiti mkubwa linapokuja suala la hatma ya Guimaraes.

# XABI ALONSO HAJAWASILIANA NA REAL MADRID



**MUNICH,** Ujerumani

WAKALA wa kocha wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso amesisitiza kuwa hawajawasiliana na Real Madrid kuhusu uwezekano wa kuhamia Santiago Bernabeu.

Majira ya joto yaliyopita, Alonso alipokuwa akiiongoza Leverkusen kutwaa ubingwa wa Bundesliga bila kupoteza, kiungo huyo wa zamani alihusishwa sana na kutaka kuondoka. Bayern Munich na Liverpool zote zilikataliwa hadharani, ilihali waajiri wenzao wa zamani Real Madrid walidokezwa kila mara kusubiri hadi 2025 ili kuanzisha harakati zao.

Hivi majuzi, ripoti ilidai Madrid wanapanga mpango wa kumnunua Alonso na kiungo nyota wa Leverkusen Florian Wirtz, wakiwa na ndoto ya kuwaleta Bernabeu msimu ujao wa majira ya joto.

Akihojiwa kuhusu nia ya Madrid kwa Alonso, wakala Inaki Ibanez alisisitiza kwamba hakuna kitu zaidi ya uvumi kwa wakati huu.

"Hakukuwa na mazungumzo yoyote na Real Madrid," aliiambia MARCA. "Historia inajirudia mwaka mmoja baadaye.


"Hatukuzungumza, hatujazungumza."

Kocha wa sasa wa Madrid, Carlo Ancelotti mwenye umri wa miaka 65, yuko chini ya mkataba hadi 2026 ingawa haiaminiki kuwa kuna nia ya haraka ya kuachana na Muitaliano huyo, inafahamika kwamba kibarua chake kinakaribia mwisho na Madrid wanaweza kuhitaji kuingia sokoni.

Liverpool na Bayern wanafurahia maisha chini ya Arne Slot na Vincent Kompany huku Chelsea, Manchester United na Barcelona zote zimeajiri makocha wapya msimu huu na kuna uwezekano mkubwa wa kuwepo sokoni.

Kazi ndani ya Manchester City pia inaonekana kukosekana mezani baada ya Pep Guardiola kukubaliana na masharti ya kuongezwa mkataba.

# Wakala afichua kuhusu Liverpool



**MANCHESTER,** England

WAKALA wa winga wa Manchester United Antony amethibitisha kuwa kuna ukweli kuhusu ripoti zilizofichuka zikielezea nia ya Liverpool ya kutaka kumsajili Mbrazil huyo mwaka 2022.

Jumanne iliyopita ziliibuka taarifa kuwa kocha wa zamani wa Liverpool, Jurgen Klopp alikuwa amezungumza na Antony, ambaye wakati huo alikuwa nyota mchanga wa Ajax kutaka kusamjili na kuwa mbadala wa Mohamed Salah, ambaye alikuwa akiingia miezi 12 ya mwisho ya mkataba wake na wakati huo alionekana anajiandaa kuondoka Anfield.

Hata hivyo, Salah alisaini mkataba mpya msimu huo ambao unamuweka klabuni hapo mpaka mwakani 2025, na Antony baadae alisaini mkataba wa awali wa pauni milioni 82 chini ya Erik ten Hag huko United.

Alipoulizwa kuhusu ripoti hiyo, wakala wa Antony Junior Pedroso alisema: "Ndiyo, hadithi hii ina msingi fulani wa ukweli.

"Salah aliongeza mkataba wake wakati huo na hilo lilifanya uhamisho wa Antony kwenda Liverpool kutowezekana."

Antony kwa sasa anapigania mustakabali wake huko United baada ya misimu miwili na Liverpool kwa mara nyingine wamejikuta wakitoa jasho kutokana na mkataba wa Salah.

Wakati huu, Salah anakaribia miezi sita ya mwisho ya mkataba wake wa sasa, kama ilivyo sasa, kuna uwezekano akajadili uhamisho wa bure nje ya nchi kuanzia Januari.

# Barcelona kurejea Camp Nou 2025

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA inatarajiwa kurejea Camp Nou Februari 2025, ESPN Imethibitisha.

Vinara hao wa LaLiga waliondoka Camp Nou mwishoni mwa msimu wa 2022/23 na kuhamia kwa muda katika Uwanja wa Olimpiki huku uwanja wao wa nyumbani ukifanyiwa ukarabati.

Walitarajia kurejea kabla ya mwisho wa 2024 lakini walithibitisha mapema msimu huu kwamba hawataweza kucheza mechi Camp Nou hadi 2025.


Akitoa muda maalum zaidi, mjumbe wa baraza la jiji David Escude alithibitisha kuwa mpango wa Barcelona ni kurejea Camp Nou ifikapo Februari.

"Tarehe iliyotolewa na makamu wa rais Elena Fort katika Bunge lililopita, ambayo ni Februari, ndiyo ambayo pia tunayo," aliiambia RAC1.

"Hakuna mabadiliko.

"Ni jambo la akili sana kwa klabu kupata tarehe chache zaidi, kwani tayari tumeshaona mvua imenyesha na kunaweza kutokea tukio ambalo halikutarajiwa, lakini taarifa tulizonazo ni za Februari."

Escude alifichua mazungumzo yake ya hivi punde na klabu hiyo yalikuja Jumatatu huku kila mmoja anayehusika akifanya kazi ili kuhakikisha mabadiliko ya kurejea Camp Nou, ambayo yanatarajiwa kufanya kazi kwa kiwango kidogo hadi mwisho wa msimu.



## Moallin ajipanga kuipaisha Yanga

INATOKA UK. 24

furaha ya kujiunga na Yanga kwa sababu ametua kwenye klabu kubwa na yenye historia ya kubeba mataji.

"Nina furaha sana kuwa Yanga, ni timu kubwa Tanzania na Afrika, naahidi nitashirikiana na wenzangu wa benchi la ufundi ili kuifanya klabu hii iendelee kuwa tishio," Moallin aliongeza.

Alilisifia soka la Tanzania limekuwa kwa kasi na kuwafanya wachezaji wengi wa nje ya nchi 'kumiminika' kuja kucheza soka la kulipwa.

"Soka la hapa limepiga hatua kubwa sana, kila mtu anaitazama Ligi Kuu ya Tanzania, haishangazi kushika nafasi ya sita Afrika, kiasi imefanya wachezaji wengi wa nje wanatamani kuja kucheza soka nchini, nadhani hili inabidi Watanzania wajivunie," alieleza Moallin.

Yanga ilianza kumtangaza Mjerumani, Sead Ramovic, kuchukua mikoba ya Miguel Gamondi na Mustapha Kodro, akiajiriwa kama Kocha Msaidizi, nafasi iliyokuwa inashikiliwa na Msenegal Moussa N'Daw.

Kwa sasa Yanga inajiandaa kuikaribisha Al Hilal kutoka Sudan katika mechi ya kwanza ya hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa Novemba 26, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

## Simba, Pamba Jiji kibaruani

INATOKA UK. 24

ina wachezaji wazuri kama Pamba Jiji, tumejiandaa kukabiliana nao, tunataka kufanya vizuri kwenye uwanja wetu wa nyumbani," alisema Minziro.

Alisema licha ya kuwa kwenye uwanja wao wa nyumbani, wataingia katika mchezo huo kwa tahadhari na wataongeza umakini ndani ya dakika zote.

Ligi hiyo itaendelea tena kesho kwa KenGold kuikaribisha Coastal Union wakati Mashujaa itawaalika Namungo na Azam itawavaa Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Azam Complex.

Simba yenye pointi 25 ndio vinara wa ligi hiyo yenye timu 16 wakifuatiwa na mabingwa watetezi, Yanga yenye pointi 24 wakati Singida Black Stars iko katika nafasi ya tatu na pointi zake 23 kibindoni huku Azam FC yenye pointi 21 wakikamilisha nne bora.

Kagera Sugar yenye pointi nane sawa na Pamba Jiji na KenGold ilijikusanyia pointi tano tu mpaka sasa ndio zinaburuza mkia kwenye ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara.

# YANGA YAFUNIKA LIGI U-20, AZAM, SIMBA ZINASUASUA

**Na Adam Fungamwangwo**

TIMU ya soka ya vijana ya umri chini ya miaka 20 ya Yanga (u-20), inaongoza katika Kundi A, ikicheza michezo minne, ikishinda mitatu, sare moja, ikifunga jumla ya mabao 13 na kuruhusu nyavu zake kutikiswa mara tatu.

Kwa mujibu wa msimamo uliotolewa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) kwa timu za vijana ambazo timu zao kubwa zipo Ligi Kuu, Yanga inafuatiwa na Azam FC yenye pointi tisa, ikicheza michezo minne, lakini ikifunga mabao tisa tu na kuruhusu matano.

Msimamo unaonyesha Dodoma Jiji inashika nafasi ya tatu ikiwa na pointi saba, huku Pamba Jiji, Tabora United, na Kagera Sugar zote zina pointi sita kila moja, Mashujaa FC nafasi ya saba ikiwa na pointi nne, na Singida Black Stars ikiburuza mkia ya kundi hilo, licha ya kucheza michezo minne, lakini haina pointi.

Kundi B linaongozwa na JKT Tanzania ambayo imejikusanyia pointi tisa katika michezo minne waliyocheza, ikishinda tatu na sare moja, ikifuatiwa na Prisons ambayo ina pointi saba.

**Simba, inashika nafasi ya tatu ya kundi hilo, ikiwa pia na pointi saba, lakini ikizidiwa na uwiano wa mabao ya kufunga na Prisons.**

Maafande hao wamefunga mabao saba na kuruhusu saba, huku Simba ikifunga matano na kuruhusu pia matano.

Coastal Union na KenGold zote zina ponti sita kila moja, Fountain Gate nafasi ya sita ikiwa na pointi tano, KMC na Namungo zina pounti tatu kila moja, lakini Namungo ikiwa mkiani kutokana na kufunga mabao manne tu, huku KMC ikifunga saba.




Mshambuliaji wa Simba Queens, Jentrix Shikangwa (katikati), akiwania mpira dhidi ya wachezaji wa Gets Program ya Dodoma katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (TWPL), iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi. Simba Queens ilishinda mabao 6-2. **PICHA: SIMBA SC**

# *Simba Queens haikamatiki TWPL*

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya timu yake kupata ushindi wa mabao 6-2 dhidi ya Gets Program, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Yussif Basigi, amesema amefurahishwa na matokeo hayo na anaamini wachezaji wake wataendelea kupambana katika kila mechi wanayocheza.

Ushindi huo umeifanya Simba Queens iliyoshinda mechi zote tano ilizocheza ifikishe pointi 15 na kujiimarisha kileleni ikifuatiwa na Maafande wa JKT Queens yenye pointi 13.

Akizungumza na gazeti hili, Basigi, alisema mechi hiyo haikuwa rahisi, anawapongeza wachezaji wake kwa kuonyesha utulivu na hatimaye kuondoka na pointi tatu muhimu katika mechi hiyo.

Basigi alisema ligi hiyo inaushindani na wao wamejipanga kucheza kila mechi sawa na fainali.

"Ligi inaushindani sana, tunaendelea kuwakumbusha wachezaji kutulia wanapokuwa na mpira, kikubwa ninawapongeza kwa kuhakikisha tunaendelea kupata ushindi, lengo letu ni kutwaa ubingwa na kushiriki mashindano ya kimataifa mwakani," alisema Busigi.

Hata hivyo, Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (TWPL), itasimama kupisha Kalenda ya Kimataifa na itarejea tena kuanzia Desemba 10, mwaka huu.

# Michezo

Ijumaa Novemba 22, 2024

Nipashe



Bruno afichua kutakiwa Man City UKURASA 21



Mabeki wa Simba, Che Malone Fondoh (kulia) na Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr', wakifanya mazoezi siku chake kabla ya kikosi cha timu hiyo kuelekea Mwanza. Simba inatarajia kukutana na wenyeji Pamba Jiji FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini humo. **PICHA: SIMBA SC**

## Moallin ajipanga kuipaisha Yanga

**Na Adam Fungamwango**

MKURUGENZI mpya wa Ufundi wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, Abdihamid Moallin, amesema ataifanya timu hiyo kuwa kubwa barani Afrika, lakini pia kuzalisha wachezaji wenye vipaji na 'kulisha' klabu nyingine duniani.

Moallin alitangaza kuachana na KMC FC inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kama Kocha Mkuu na kutua rasmi Jangwani mapema wiki hii.

Akizungumza kwa mara ya kwanza baada ya kupewa nafasi hiyo, Moallin, alisema lengo lake kubwa ni kuzalisha wachezaji vijana wenye vipaji, kwa sababu yeye ni muumini mkubwa wa kutumia nyota chipukizi.

"Lengo ni kuendelea kusaidia kuijenga klabu hii kubwa kwa mwelekeo sahihi, nataka tuwekeze kwa vijana kufanya akademi yetu kuwa moja ya vitalu bora nchini na Afrika kama ilivyokuwa Asec Mimosas ya Ivory Coast.

Tunataka kuzalisha wachezaji bora kwa ajili ya timu yetu ya kwanza na timu ya Taifa ya Tanzania kwa ujumla, lakini kulisha timu nyingine nje ya nchi ili wacheze mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema Moallin.



Bosi huyo mpya alisema mbali na kuzalisha wachezaji kwa ajili ya timu kubwa ya wanaume, lakini pia lengo lake ni kuimarisha kikosi cha Yanga Princess ili iwe ni timu ya ushindani tofauti na ilivyo sasa.

"Tunataka pia kuimarisha pia timu yetu ya wanawake ili nayo ianze kuwania mataji, ili iwe moja ya timu bora Afrika, iliteke soka la Tanzania na kucheza mechi za kimataifa, hasa Ligi ya Mabingwa Afrika ya Wanawake," alisema mkurugenzi huyo wa ufundi.

Aliongeza amekuwa na

INAENDELEA UKURASA 23

# Simba, Pamba Jiji kibaruani

### Fadlu afunguka mechi hiyo ni kipimo kizuri kwao...

**Na Faustine Feliciane**

SIMBA inatarajia kuutumia mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Pamba Jiji FC utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza kama sehemu ya maandalizi ya mechi ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, imeelezwa.

**Mechi hiyo ya kwanza ya hatua ya makundi ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya wageni FC Bravos do Maquis kutoka Angola itachezwa Novemba 27, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amesema mchezo dhidi ya Pamba Jiji kwao ni kipimo na maandalizi mazuri zikiwa zimebaki siku chake kukutana na Bravos do Maquis.

Fadlu alisema baada ya mapumziko mafupi ya Kalenda ya Kimataifa kumalizika, walihitaji angalau mchezo mmoja wa ushindani na wanafurahia kukutana na Pamba Jiji kwa sababu itawajenga wachezaji wake.

Kocha huyo alisema amejiandaa kukutana na upinzani katika mechi hiyo kwa sababu anafahamu ni 'hatari' kukutana na timu ambayo haina matokeo mazuri katika michezo yake iliyotangulia.

"Mchezo huu wa kesho (leo), ni muhimu sana kwetu, kwanza tunataka kuendelea kujiimarisha kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu, lakini pia ni sehemu ya maandalizi yetu kuelekea mchezo wa kimataifa," alisema Fadlu.

Kocha huyo alisema wamejiandaa vizuri na mchezo huo na wanafahamu Pamba wataingia uwanjani kuonyesha upinzani wakijaribu kutafuta ushindi wa kwanza kwenye uwanja wao wa nyumbani.

"Hautakuwa mchezo mwepesi hata kidogo, Pamba wana kocha mzuri na wachezaji wazuri pia, lakini sisi lengo letu ni kuondoka na pointi tatu, ushindi utatuongezea morali zaidi kuelekea katika mchezo wetu wa kimataifa wa CAF," alisema Fadlu.

Aliongeza wachezaji wake wapo katika hali nzuri na hata waliotoka kwenye majukumu ya kimataifa pia wako tayari kwa ajili ya mchezo huo.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amewataka waamuzi wa mchezo huo kuwa makini na kuwaepusha wachezaji wao kuumia.

"Tunaomba Pamba wacheze mpira, wasiingie uwanjani kwa lengo la kuwaumiza wachezaji wetu, tuna mchezo mkubwa wa kimataifa, waamuzi nao wawalinde wachezaji wetu, tuache soka lichezwe uwanjani si kukamiana na kuumizana," alisema Ahmed.

Naye Kocha Mkuu wa Pamba Jiji, Fred Minziro, ameliambia gazeti hili anaiheshimu Simba kutokana na kuundwa na wachezaji wenye uzoefu lakini watahakikisha wanapambana kupata pointi tatu.

"Simba ni timu kubwa na

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >